ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

		na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais

16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe

32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano - Tarehe 13 Februari, 2018

Kikao kilianza saa 3:00 (Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, Katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma aliuliza swali namba 12 kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa mnasaba huo kutokana na majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Salha aliuliza swali la nyongeza na kujibiwa swali hilo.

Hata hivyo, Mhe. Machano Othman Said alikuwa na wasiwasi juu ya majibu hayo na aliomba swali hilo lijibiwe tena ili upatikane usahihi wake kwa mujibu wa Kanuni ya 37 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto asome jibu la swali hilo ili kuweka sawa taarifa rasmi ya Baraza "Hansard".

Mhe. Spika**,** wakati ninajibu swali Namba 12, niliulizwa swali la nyongeza na Mheshimiwa Salha Mohamed Mwinjuma aliyetaka kujua idadi ya vijana waliopatiwa mikopo kwa Unguja na Pemba.

Jibu la suala hilo kwa usahihi na kuweka hansard vizuri ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 jumla ya shilingi 600,000,000/- zilizotolewa mikopo na Mfuko wa Uwezeshaji ambapo shilingi 390,000,000/- zilikwenda kwa vijana 2,267 katika mikoa mitano ya Zanzibar, kati ya vijana hao vijana 1,260 ni wanawake na 1,007 ni wanaume.

Kimikoa fedha hizo zilitolewa kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Kusini Pemba	Shilingi 37,857,300/- kwa vijana 290 (wanawake 108, wanaume 122).
Mkoa wa Kaskazini Pemba	Shilingi 36,140,000/- kwa vijana 190 (wanawake 93, wanaume 97).
Mkoa wa Mjini Magharibi	Shilingi 168,493,650/- kwa vijana 569 (wanawake 330, wanaume 239).
Mkoa wa Kaskazini Unguja	Shilingi 58,359,500/- kwa vijana 200 (wanawake 112, wanaume 88).
Mkoa wa Kusini Unguja	Shilingi 93,149,550/- kwa vijana 1018 (wanawake 557, wanaume 461)

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 42

Kiwanda Cha Ufundi Seremala Saateni

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa kikosi cha JKU kina miradi mbali mbali ya uzalishaji mali kama mashamba kwa ajili ya kilimo, mifugo, ulinzi n.k na kwa sababu kikosi cha JKU kinacho kiwanda cha ufundi Seremala Saateni ambacho kilikuwa kinazalisha na kuuza fanicha za aina mbali mbali.

(a) Je, kiwanda hicho bado kipo na kinafanya kazi kama zamani.

(b) Je, kiwanda hicho hupokea vijana wangapi kwa mwaka ambao huwapatia ujuzi wa ufundi seremala.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kilikusanywa na JKU kutokana na kazi zinazofanywa kiwandani hapo kuanzia mwaka 2015/2017.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 42 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Kiwanda cha Seremala cha JKU kimeanzishwa kabla ya Mapinduzi ambapo wakati huo kulikuwa na kiwanda cha Fanicha A kilichomilikiwa na Kampuni ya Patel na Kiwanda cha Fanicha B kilichomilikiwa na Kampuni ya Ex Karampa. Baada ya Mapinduzi Matukufu kiwanda hicho kilitaifishwa na kuwa chini ya Wizara ya Elimu mwaka 1964 hadi mwanzoni mwa miaka ya 70. Baada ya hapo kiwanda hicho kilikabidhiwa Wizara ya Biashara hadi mwaka 1989 kilipokabidhiwa rasmi kwa JKU kwa ajili ya mafunzo kwa vijana wa uzalishaji wa bidhaa za Fanicha.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kiwanda cha Useremala kipo na kinafanya kazi kama kilivyokusudiwa. Kwa ujumla hali ya uzalishaji ni nzuri na bidhaa zinazotengenezwa ni pamoja na vitanda, makabati, madawati, meza na viti vya Ofisi na vya nyumbani.

(b) Mhe. Spika, wastani wa vijana 50 hupokelewa kwa mwaka kutoka Chuo cha Mtoni baada ya kukamilisha mafunzo yao ya nadharia. Idadi hiyo ni kwa mujibu wa uwezo wa kiwanda chenyewe.

(c) Mhe. Spika, jumla ya shilingi 60,000,000/- zilikusanywa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017 kutokana na makusanyo ya kazi za ndani na nje Mhe. ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo nyongeza kwa kuwa umesema katika jibu lako vijana takriban 50 hupokelewa kwa kila mwaka na kwa idadi hiyo inaonekana sasa tushapata vijana wengi.

a) Je katika hicho kiwanda kwa sasa hivi kuna mafundi wangapi ambao wanafanya kazi hizo za huo ufundi seremala

b) Kwa kuwa kazi hiyo ya ufundi seremala inaendana na sambamba na kazi ya uwezekaji na mambo mengine finishing ya juu jee kuna mafundi wangapi uliowapata kutokana hapo Saateni ambao wanautaalamu wa ujenzi wa juu wa majengo ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kutowa majibu ya nyongeza ya Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli idadi ya vijana ambao wanatolewa ni ukweli usiofichika kwamba tumeweza kuongeza vijana ambao wanaweza kupata ujuzi huo, lakini naomba nitowe majibu kutokana na suala lake la kutaka kujuwa ni idadi ya mafundi wangapi naomba nitowe maelezo.

Mhe. Spika, mafundi tulokuwa nao ni maaskari wetu ambao wametokana na miongoni mwao wametokana na ujuzi wao, katika sehemu zao ambazo wao wenyewe walipata ujuzi kutokana na sehemu zao ambazo wametoka na miongoni mwao wapo ambao wamejifunza kwa kupitia viwanda vyetu ambavyo kiwanda chetu hicho.

Sasa ukweli ni kwamba unapozungumzia fundi tunachoangalia zaidi ni utaalamu kwa kuwa sina taarifa au sina takwimu sahihi kwamba mafundi hao labda wametoka wamesoma kwa *level* gani na siwezi kuthibitisha kwamba tuna mafindi idadi kiasi gani kutoka na fundi ni lazima apite kwenye chuo. Nimuombe Mhe. Mwakilishi, baada ya kutoka hapa, basi anifate tutafanya juhudi ya kuona tunampatia majibu yaliyo sahihi kutokana na takwimu ambayo amezitaka tuzitowe.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika swali mama imeelezwa wazi kwamba JKU inamiliki mashamba mengi mimi nina swali dogo la nyongeza. Inaonekana mashamba yale hayajafikiwa lengo hasa ya kilimo kinachotakiwa ya vikosi vya JKU.

a) Mhe. Waziri anaweza kuniambia ni kwanini hayakufikiwa lengo lile lililokusudiwa

b) Na ikiwa hayakufikiwa kuna mpango gani wa kuhakikisha mashamba yale yanafikiwa lengo lile na sababu gani ambazo zimefanya yasifikiwe kiwango kile kinachotakiwa cha asilimia mia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza naomba kwa ruhusa yako naomba ningeomba Mhe. Mwakilishi swali lake alirejee lakini sambamba na hilo nilikuwa naomba kidogo kwamba swali hili lilikuwa linaelekeza zaidi katika maswala ya Kiwanda sasa naomba Mhe. maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza nataka nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa swali mama ambalo limeletwa linalohusu swali la Kiwanda cha uchongaji kwa kulijibu vizuri na hili swali la Mhe. Hamad Abdalla Rashid linahusu zaidi mashamba na sio Kiwanda wakati swali mama lilikuwa linahusu Kiwanda cha Uchongaji, hata hivyo kwa sababu wewe ndio mwenye mamlaka Mhe. Spika, umeturuhusu tulijibu swali hili.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Hamad Abdalla Rashid, kwamba mashamba yote yanayomilikiwa na JKU. JKU inayaendeleza vizuri na inayalima vizuri na kwa yale maeneo ambayo kwa mujibu wa uwezo wa matumizi ya fedha ya JKU wanayopangiwa ya kiwa hawana uwezo wa kuweza kuyalima huwa tunawaazima wananchi kwa madhumuni ya kuwapa wananchi kujipatia kipato.

Hata hivyo, JKU inao mpango madhubuti kabisa kupitia mpango mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuyalima na kuyaendeleza mashamba hayo ahsnte sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, mimi nilikuwa pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nilikuwa nataka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Viwanda vya Saateni mashine zake nyingi ni mashine za kiasili, za zamani na sasa hivi tumekuwa tumeingia katika wakati wa *technologia*. Je Wizara imejipanga vipi katika kununuwa mashine za kisasa ambazo ni za *technologia* ili kuweza kutowa vifaa vyenye ubora zaidi ili kuweza kuingia katika ushindani wa kibiashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba mashine ambazo tulokuwa nazo sio zile za kisasa kama ambavyo Mhe. Mwakilishi ameweza kuzungumzia lakini hata hivyo, Wizara kupitia JKU inawo mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba na sisi tunaingia katika ushindani katika fani hizi za viwanda kwa hiyo kiufupi tunachotegemea hapa ni kutokana na bajeti zetu ambazo jinsi ambavyo zitakuwa zimeruhusu basi ndio hivyo hivyo tutakuwa tukifanya juhudi kuona kwamba tunatafuta uwezekano kupata mashine ambazo zinaendana na hali ya kisasa ili kusudi na sisi tuweze kukabiliana na ushindani uliopo hapa nchini Mheshimiwa ahsante.

Migogoro Baada Ya Kuvunjika Kwa Ndoa

Mhe. Omar Seif Abeid -Aliuliza**:**

Kwa kuwa siku hizi ndoa nyingi kwa vijana huvinjika muda mfupi baada ya kufungwa, jambo ambalo halipendezi sio tu kwa wazazi wa vijana hao bali hata kwa jamii na Serikali kwa ujumla kwani kuvunjika kwa ndoa hizo husababisha upande mmoja wa ndoa hiyo kupata shida ya kutunza familia iwapo mke alishapata mtoto au ujauzito ndani ya ndoa na hatimae huzuka migogoro na kupelekana mahakamani kwa kosa la matunzo au kugombania mtoto.

(a) Je, serikali haioni kwamba kutokana na sababu hiyo na nyenginezo ipo haja kwa sasa kuweka sheria itakayoweza kuzilinda ndoa hizo zisivunjike ovyo ovyo kama ilivyokuwa kwa wazee wetu hapo zamani.

(b) Je, ni ndoa ngapi kwa kipindi cha 2015/2017 ambazo zimeripotiwa kufungwa na talaka zimesajiliwa.

(c) Je, ni migogoro mingapi ya talaka na madai ya matunzo ya watoto yaliyoripotiwa katika Mahkama za Kadhi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake lenye Nam. 35 lenye vipengele (a)**,** (b) na (c) kabla ya kumjibu kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo**:-**

Mhe. Spika, kazi kubwa ya Mahkama ni kupokea kesi, kusikiliza kesi na kutoa uamuzi kwa kufuata taratibu za Sheria zilizowekwa. Hakuna mamlaka/sheria yoyote ile iliyopewa Mahkama kusajili ndoa au talaka. Uozeshaji wa ndoa Zanzibar hufanywa na

wasajili wa ndoa kwa mujibu wa Sheria kwa mfano, Masheikh, Makadhi, Mapadri na Watendaji wa wakuu wa Mikoa, nk. Uozeshaji huo hufanyika maeneo tofauti. Mahkama haihusishwi kabisa katika uozeshaji na usajili wa ndoa hizo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali Nam. 35 lenye (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika**,** kama tunavyoelewa wananchi wengi wa Zanzibar ni waislamu, itakuwa ni vigumu kuweka sheria ambayo itakayomzuia mwanandoa (mume) kutoa talaka na itakuwa imeenda kinyume na Sheria zilizowekwa na dini ya kiislamu. Hata hivyo ili kulinda ndoa zisivunjike ovyo ovyo ni jukumu la jamii nzima kuelimisha wanandoa ili waweze kustahamiliana ili ndoa hizo zisivunjike.

(b) Mhe. Spika, swali hili linaweza kujibiwa na taasisi yenye jukumu la kusajili ndowa na talaka ambayo ni Idara ya Vizazi na Vifo ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikowa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum naomba nimshauri Mhe. Omar Seif Abeid awasiliane na Mhe. Waziri anayehusika wa Idara hiyo.

(c) Mhe. Spika, Takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa kesi za madai ya Talaka zimezidi kuongezeka katika Mahkama za Kadhi Unguja na Pemba ukilinganisha na kesi za madai ya matunzo ya watoto.

Mhe. Spika, kwa upande wa madai ya talaka takwimu zinaonyesha kuwa kesi zilizofunguliwa Unguja jumla ni 884, kesi 440 zimetolewa uamuzi na kesi 444 bado zinaendelea, kwa upande wa Pemba kesi zilizofunguliwa ni 334, kesi 249 zimetolewa uamuzi na kesi 85 bado zinaendelea.

Mhe. Spika, katika kesi za Madai ya matunzo ya watoto takwimu zinonyesha kesi zilizoripotiwa Unguja jumla yake ni 35, kesi 17 zimetolewa uamuzi na kesi 18 bado zinaenelea. Kwa upande wa Pemba kesi zilizoripotiwa ni 22, kesi 18 zimetolewa uamuzi na kesi 4 bado zinaendelea nashukuru.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Waziri maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa umekiri kwenye jibu lako kwamba kwa upande ya talaka takwimu zimeongezeka.

Mhe. Spika, samahan, kwa kuwa amekiri kwamba kesi za talaka zimeongezeka kwa upande wa Unguja tatizo ambalo ndilo jamii sasa inalolia nalo nayeye amesema kwamba hakuna utaratibu pamoja na kuwa ni waislamu lakini kuna wengine ambao si Waislamu hawana Dini, na wengine
wana Dini tofauti, na jambo hili sasa hivi mheshimiwa ukitaka kwenda popote anasema kwamba twende vizazi na vifo ili kutaka kujua takwimu.

a) Lakini je, haoni kama huo ucheleweshaji wa hizo kesi zilizotajwa hapa kwa upande wa Unguja kwamba ni tatizo kwa upande unaolalamika kukosa kupata haki yake kwa wakati unaostahiki.

b) Kuhusu habari ya kesi za matunzo ya watoto je, sambamba na hili haoni kwamba wale wanawake wenye watoto ambao wamekoseshwa matunzo ya watoto wale kuwacheleweshea ni kuwadhiki katika maisha yao kwa ajili ya hali ngumu ya malezi ya watoto hawa. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako

naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b), lakini nitajibu kwa pamoja.

Mhe. Spika, swali la uendeshwaji wa kesi na ucheleweshaji wa kesi ni suala ambalo sio kwamba linafanywa makusudi, kunakuwa kuna mambo mbali mbali ambayo yanapelekea kesi zile kuchelewa. Lakini nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba jitihada zinaendelea kuhakikisha kesi hazichukui muda mrefu na wale wote ambao wanakuwa na haki ya kupewa kesi hizo wanazipata kwa wakati. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimpongeze kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa, lakini naomba nimuulize swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa uvunjikaji wa wana ndoa hawa au ndoa hizi ambazo zinafungwa katika jamii zetu kunasababisha ukosefu mkubwa wa elimu. Je, serikali ina mpango gani wa kujenga madrassa ama skuli kwa wanandoa hawa ili kuweza kupata elimu kwanza kabla ya ndoa.

b) Kuna utafiti gani ambao mmeufanya kama serikali kujua ni wanandoa gani ambao wanasababisha kuvunjika kwa ndoa hizi kati ya wanawake au wanaume. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, suala la uvunjikaji wa ndoa kwa maana ya kwamba watu hawa wanahitaji kupewa elimu. Elimu inatolewa ushahidi huo upo, wizara yetu kupitia taasisi zake mbali mbali kama vile Ofisi ya Mufti imekuwa

mstari wa mbele kutoa elimu mbali mbali ikiwemo elimu ya ndoa. Kama tuelewavyo kwamba Mashekhe wetu huwa wanapata fursa ya kuonana na watendaji wetu wa ofisi ile muda tofauti na sehemu mbali mbali ili pamoja na mambo mengine kubadilishana mawazo na kukutana na wale walengwa na vile vile hata katika hotuba zetu za Ijumaa, basi huwa tunapata fursa vile vile kutoa elimu ile. Kwa hivyo, kiufupi mheshimiwa elimu ya ndoa kwa njia moja au nyengine inatolewa na taasisi zetu mbali mbali zinazohusiana na masuala ya ndoa.

b) Mhe. Spika, pia niseme kwamba hadi sasa hivi hakuna utafiti rasmi ambao umefanyika unaonesha kwamba kama wanandoa wanawake ndio ambao wanasababisha mtafaruku huu au wanaume. Kwa hivyo, hili bado utafiti haupo rasmi kusema kwamba wanawake ndio wanasababisha ndoa kuvunjika au wanaume wanasababisha ndoa kuvunjika. Lakini niseme kwamba ni vyema kama jamii basi tukae vizuri katika jamii tupendane katika jamii, mume ampende mke na mke ampende mume ili ndoa hizo ziweze kudumu kwa muda mrefu na watoto wetu waweze kupata huduma kwa wazee wao wote hao wawili. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kwa sababu ndio nasema tena *Bismillahi Rahman Rahiim.* Namuuliza Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri ni kwamba kwa sasa hivi kwa kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein tunaipa kazi kubwa sana kwa ajili ya kuwalea watoto ambao mayatima na wengine wenye baba waliokuwa hawawashughulikii, hii husababishwa na ndoa ambazo zinakuwa hazina mashiko. Je, nimuulize Mhe. Naibu Waziri tuna mikataba ambayo tunaifunga kwa kuzingatia tu kwamba tunataka ushahidi wa ndoa kama kakuoa au umeolewa, lakini hakuna udhibiti wa

kwamba pale baada ya ndoa kunatokea kitu chengine cha mtoto kwamba yule mtoto atakuwa ana malezi ya kiasi gani pale.

a) Je, tuna utaratibu gani kwa mwanandoa ambaye kama ni baba ambaye ameoa atakapomuacha mtu yule kama ni mfanyakazi wa serikali anakatwa *percentage* gani ili kupelekewa mtoto kama wameachana na mama yake.

b) Ni kwamba kwa mazoea tumekuwa na ndoa za miezi hasa wakati wa Shaaban kwa ajili ya kufunga. Je, suala hili umeliona maana yake baada ya Ramadhan Mfunguo Mosi tunaacha na wakati wengine wameshakuwa na vitumbo. Je, serikali imechukua hatua gani kuhusu habari hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa hivi sasa hakuna utaratibu pale ambapo mume anapomuacha mke kukawa kuna *percentage* fulani kwamba mke yule aweze kuipata kwa mumewe.

b) Mhe. Spika, suala la kuhusina na ndoa za mwezi kwa maana ya kwamba mwezi wa Shaaban watu wanaoana na Mfunguo Mosi wanaachana. Hii nirejee kusema kwamba tujitahidini katika ndoa zetu na tujenge uvumilivu katika ndoa zetu na vile vile tujifunze siri gani wazee wetu wa zamani na wengi wetu wazee wetu mpaka dakika hii hawajaachana na sisi tumeshakuwa watu wazima humu, iweje mtu unaoa leo kesho uache, hapa pana kasoro. Kwa hivyo, kubwa zaidi tusome siri ya mafanikio ya wazee wetu ndoa zao kudumu kwa muda mrefu. Ahsante.

Nam. 18

Upungufu wa Maji Katika Baadhi ya Maeneo ya Mji wa Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika jitihada zake za kuleta maendeleo kupitia miradi ya maji. Pamoja na jitihada zote bado kuna baadhi ya maeneo maji hayapatikani ipasavyo kama vile mji wa Chake Chake katika eneo la Chanjaani, Matuleni, Chanjamjawiri na Kiziwani Shungi yanayosababishwa na kutokuwepo kwa "*reserve tank*" lililo juu kwa ajili ya kusambaza maji maeneo ya mbali na kusababisha mashine za kupandisha maji kufanya kazi kwa muda mrefu na mashine hizo hazichukui muda mrefu huharibika

(a) Je, katika vijiji hivyo nilivyovitaja vyenye ukosefu wa maji ya *ZAWA*, wizara inachukua hatua gani za dharura na za muda mrefu ili wananchi hao wapate huduma hiyo.

(b) Je, kama huduma hiyo inaweza kuwa ngumu kulitatua tatizo kwa haraka, tunaweza tukashirikiana kuwachimbia visima ili kutatua tatizo la maji katika maeneo hayo.

(c) Eneo la Chake Chake linaonekana kuwa na upotevu wa maji kiholela, kwa tathmini ya *ZAWA*, asilimia ngapi ya maji hayo yanapotea na hatua gani zimechukuliwa za kuondoa matatizo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, Zanzibar tayari imekwishapata fedha kutoka serikalini kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa mradi wa maji wa Matuleni ambapo miongoni mwa vijiji vitakavofaidika ni Matuleni, Chanjamjawiri na Kiziwani Shungi na matayarisho ya utekelezaji kazi yanaendelea.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inakaribisha mdau yeyote kwa maendeleo wa ndani na wa nje ya nchi katika kuimarisha huduma ya maji mijini na vijijini hasa kwa eneo la Chanjaani Chake Chake.

(c) Mhe. Spika, wastani wa asilimia 30 ya maji yanakadiriwa kupotea kutokana na mivujo pamoja na utumiaji wa maji usio halali. Jitihada zinazochukuliwa ni pamoja na kufanya ukaguzi na matengenezo katika maeneo yanayolalamikiwa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi leo nishukuru na kumpongeza zaidi Naibu Waziri kwa kunipa moyo na pia wananchi wangu wa Chake Chake pamoja na Kiziwani kufurahi maana yake tokea Mapinduzi haya ya serikali hii yaanze eneo la Kiziwani hawajapata maji, lakini najua muarubaini wake uko karibu.

a) Mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri ni kipindi gani ambacho kitakuwa tayari kwa matengenezo katika maeneo ya Chanjamjawiri na Kiziwani.
b) Katika Mji wa Chake Chake kama ulivyosema asilimia 30 maji yanapotea. Ni kweli mji wote unaukuta unarishai maji, mnafanya mapitio ya muda gani au kila kipindi gani katika maeneo ili kuangalia kwamba maji hayapotei.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Tunategemea mwishoni mwa Machi, tukijaaliwa kazi itakuwa imekamilika na huduma imewafikia wananchi.

b) Lakini kipindi gani tunakuwa tunapita hii ni kazi ya kila siku, lakini iwapo watu wetu hawajapitia katika sehemu husika tunawaomba wananchi watoe taarifa pale ambapo kuna mivujo. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba pia nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Pamoja na majibu yake naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa muda mrefu wananchi wa Mfenesini, Kama, Chuwini wana matatizo makubwa ya maji na sababu kubwa kwanza matangi mawili ambayo yako Kama ni mabovu na moja limeanguka. Pili, mabomba makuu ya maji yamepasuka zaidi ya mwaka na hayajazibwa. Je, serikali inawaahidi nini wananchi wa maeneo haya katika uzibaji wa yale mabomba lakini pia kujenga upya matenki ambayo yako Kama na yameanza kuanguka.

b) Katika ziara ya Mhe. Rais ambayo aliifanya katika Wilaya ya Magharibi "A" alipata fursa ya kutembelea visima tisa kikiwemo kisima kikubwa kwa Zanzibar katika eneo la Bumbwisudi, lakini kwa habari za chini chini kwamba visima vile vinatakiwa vipeleke maji Mji Mkongwe. Je, serikali ina mpango gani alau wa kutoa visima vitatu kwa wananchi wa Jimbo la Mfenesini wakati mradi ule utakapozinduliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kuhusiana na mvujo kama nilivyosema kawaida watu wetu wanakuwa wanapita na pale ambapo hawajapita na yanavuja basi ni vyema taarifa ifike. Lakini kwa leo hii nikuombe na nikuahidi kwamba mimi nitafika panapo majaaliwa pamoja na wataalamu wa *ZAWA* kuona namna gani yanavuja na ikiwezekana nitakuomba tushirikiane pamoja na wewe kama ambavyo Mhe. Mbunge wa Chaani nitaondoka nae baada ya kuomba ruhusa hapa.

b) Mhe. Spika, lakini kikawaida visima vinakuwa vinachimbwa kwa maeneo na vile ambavyo vimechimbwa pale vilitegemewa vipeleke maji eneo fulani, na tunategemea mwezi wa Aprili vimalizike Inshaallah katika kazi iliyobakia. Sasa maeneo hayo ambayo umeyataja kama yana upungufu kwanza tukaangalie haja kuwe na mpango wake mwengine, si vyema maji ambayo yamekusudiwa kupelekwa huku itakuwa hatujatatua tukipeleka kwengine. Nadhani umenielewa na tutashirikiana na wewe kuona namna gani tunaweza tukafanya mbadala. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa umuhimu wa swali hili nitazidisha zaidi watu wawili baada ya huyu wa tatu ambaye ameuliza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kutambua kwamba Welezo maana yake ni *well zone* eneo la visima, lakini nina masikitiko mheshimiwa huko *well zone* kama ulivyokutamka ndiko kunako mivujo mingi na *ZAWA* wanaripotiwa lakini hawaendi kuiweka sawa mivujo hiyo. Chakusikitisha zaidi huko *well zone* maji ndiko yanakoanzia lakini yanavuja na mengine yanakwenda Mjini wale wananchi wa Welezo hawapati. Hiyo mivujo ambayo umeisema iko mingi lini mtaikamilisha mivujo hiyo iondoke yote ili wale wananchi wapate maji. Maana yake Mhe. Spika, inashangaza maji yapo lakini yanavuja wananchi hawayapati, sasa lini mivujo hiyo mtaiweka sawa, mtaweka mabomba mapya ili wananchi ile mivujo imalizike na wananchi wapate kufaidika na maji hasa Welezo. Maana yake chakushangaza maji yaanaza Welezo…

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali la pili…

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Taarifa tayari hata mimi ameshanipatia lakini yeye mwenyewe Mhe. Mwakilishi amenambia nimsubirie ili twende pale Welezo, kama ameshakuwa tayari hata kesho tunaweza tukenda pamoja na wataalamu kwa sababu lazima tuone ni kiwango gani yanavuja, ni wapi yanavuja na gharama zake ni zipi. Siwezi kusema tu hapa tutafanya leo au sasa hivi au kesho kwa sababu lazima mpaka tukaone. Kwa hiyo, utayari wake maana yake utatusababishia tufike kwa haraka na mimi namsubiri yeye tu kama tulivyokuwa tumeagana. Ahsante sana.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa wanazozichukua kusaidia wananchi ili tuondokane na suala zima la maji. Lakini naomba Mhe. Naibu Waziri nimuulize swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri katika Shehia ya Mgagadu ni juzi tu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya jitihada zake kuona kwamba pale wananchi wetu wamejengewa tangi la maji kwa kusaidiwa na mradi wa wenzetu wa China, lakini ni jambo la kusikitisha sana kwamba kwa muda mfupi sana sasa hivi wananchi wa Mgagadu maji hawapati. Je, tangi lile limeshakuwa na mvujo.

b) Ni lini wananchi wale wataweza kupata huduma nzuri ya maji kuona kwamba wameondokewa na tatizo lile. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kwa bahati mbaya nisme ndio kwanza naipata hii taarifa, sasa kwa heshima naomba niichukue na niifanyie kazi na nitamjuilisha kila hatua. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Naomba niwape watu wawili, kwanza Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil halafu baadae Mhe. Jaku Hashi Ayoub.

Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na kuonesha muda wa upendeleo. Kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu laini na yenye kuleta matumaini kuhusu suala la maji.

Kwa kuwa wananchi wa Chukwani katika maeneo ya juu kuanzia Msikitini Muslim mpaka kuelekea Intebe kwa kipindi cha miaka yote hawapati maji salama na matamu. Wananchi wa maeneo yale wanajitahidi sana kuchimba visima lakini wanakumbana na maji ya chumvi. Je, wizara inao mpango mahsusi na matumaini ili kuweza kuchimba kisima na wananchi wa Chukwani juu kuanzia Muslim mpaka Intebe kupata maji safi na salama na kwa kuwa mji unakua kwa sehemu kubwa. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Niseme katika Jimbo la Chukwani tayari nimefanya ziara pamoja na Mhe. Mwakilishi husika wa jimbo lile na pale tunavyo visima vya Ras el Khaima ambavyo vipo kwenye mpango wa kuunganishwa. Sasa sijui tu huko ambako anakosema kama *plan* yetu vimehusika pamoja na hivyo, nitachokuomba tena kwa sababu sikulipata lile wakati nipo na Mhe. Mwakilishi kwa kuamini kwamba tukiviunganisha vile Chukwani yote itakuwa inapata maji tukae tena kitako ili tuone hilo eneo liko wapi lakini tufanye. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikupongeze kwa dhati kabisa kwa umakini wako wa hali ya juu jinsi ulivyoona suala hili lilivyoguswa kwa wananchi na ukaweka Kanuni kando kuuliza maswali manne, nikupongeze kwa dhati kabisa Mhe. Spika na hili ndio kilio kikubwa. Kama ninavyosema siku zote kila kitu kinatokana na maji na maji ndio *engine* ya kila kitu *wakulshaini minalmay hai.*

Mhe. Naibu Waziri uliwahi kujibu swali hapa ukasema serikali haiogopi hasara kwa wananchi wake na rekodi ninazo. Je, ni lini tutafuatana mimi na yeye kwenda Jambiani, Muungoni na Jozani

akaone ile hali, watu wa miaka mitatu na minne. Sitaji Michamvi aah! Michamvi nafikiri tena wanasubiri kudra ya Mwenyezi Mungu tu itapofika pamoja na kisima cha chumvi walichochimbiwa kile na chumvi wanayo ya kutosha tunashukuru. Ni lini tutafuatana mimi na yeye kwenda Kitogani, Muungoni, Jambiani na Jozani. Nimuombe hili swali langu dogo tu, twende mimi na fundi wake pia kwenda kuona hali halisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Tukipata nafasi wakati wowote tutakwenda, lakini pana haja sasa mimi na Mhe. Waziri na yeye tukae, kama ni lazima mimi basi tupange nafasi, tuombe ruhusa hapa tutakwenda wakati wowote tukipata nafasi au kama Mhe. Waziri atakuwa ana nafasi ya kwenda. Lakini wizara kwa ujumla iko tayari wakati wowote ilimradi tu tukipata ruhusa hapa tutakwenda. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza niendelee kushukuru majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini nimesimama kwa ajili ya ufafanuzi wa nyongeza ya mwisho ya Mhe. Jaku Hashim ya kusema kwamba watu wa Michamvi wasubiri rehema ya Mungu katika suala la upatikanaji wa maji.

Ninachotaka kumwambia Mhe. Jaku Hashim kwamba watu wa Michamvi hawatasubiri rehema ya Mungu, isipokuwa naomba nichukue nafasi hii kumkumbusha Mhe. Jaku Hashim kama alikuwepo katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed

Shein alikuwa mgeni rasmi katika mkutano ule. Miongoni mwa mambo ambayo ya msingi aliyasema yeye akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ni ahadi yake kwamba watu wa Michamvi watapata maji safi na salama katika uongozi wake kipindi hiki kabla ya mwaka 2020.(*Makofi*)

Kwa hivyo, ninachomthibitishia Mhe. Jaku Hashim kwamba ahdai ya Mhe. Rais itatekelezwa kwa nguvu zote na watu wa Michamvi watapata maji kwa miongozo na maelekezo ya Mhe. Rais bila ya kutegemea rehema ya Mungu. Tutamtegemea Mwenyezi Mungu kwa imani yetu kwamba yeye ndiye muweza wa kila jambo, lakini ahadi ya serikali itatekelezwa na watu wa Michamvi watapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana Mhe. Jaku Hashim. Mhe. Naibu Waziri nakushukuru sana kwa ustahamilivu na kuweza kujibu vizuri sana haya maswali.

Nam. 14

Mabaraza ya Vijana Katika Kupambana na Maisha

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Tangu kuanza mabaraza ya vijana na kuanza kuunda vikundi mbali mbali ndani ya sheria nyingi zimeunda vikundi vya kujiendeleza kimaendeleo na kuwafanya vijana hawa kuwa pamoja ili waweze kubuni mbinu zaidi za kupambana na maisha.

(a) Je, wizara imeweza kutembelea vikundi vingapi vya vijana kwa mwaka 2017/2018.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kimetolewa na serikali kwa Baraza la vijana kwa mwaka 2017/2018.

(c) Je, ni vikundi vingapi vimesajiliwa tangu yaanze mabaraza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kipindi cha Robo ya Pili ya Utekelzaji wa Mwaka 2017 - 2018, imeweza kutembelea vikundi 37 kutoka Wilaya zote za Zanzibar, ambapo Unguja vikundi 24 na Pemba vikundi 13 vya vijana vilitembelewa.

Vikundi hivyo vimekuwa vinajishughulisha na shughuli mbali mbali za kiuchumi, ikiwemo kilimo cha mboga mboga, ufugaji, ushonaji, uchoraji na ujasiriamali wa kutengeneza bidhaa mbali mbali. Aidha, ziara hizi zilishirikisha maafisa mikopo na ushirika katika kila wilaya, ambapo walitoa ushauri wa hatua za usajili na mikopo kwa vikundi vilivyokuwa havina taarifa hizo.

(b) Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Vijana Zanzibar katika kutekeleza kazi zake lilitengewa Ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Moja (100,000,000/=). Hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2017 Baraza la Vijana Zanzibar limepatiwa jumla ya Shilingi Milioni Sitini na Moja Laki Mbili na Elfu Arubaini na Nne (61,244,000/=).

(c) Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto tayari imekwishaanzisha Mabaraza ya Vijana ya Shehia kwenye Shehia zote, Wilaya na Taifa. Baada ya kuanzishwa kwa Mabaraza hayo hayahitaji tena kusajiliwa kama vikundi bali yatabaki kama ni taasisi zinayoweza kufanya shughuli zake mbali mbali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Saada Ramadhani Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika, namshukuru kwa majibu yake Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini kama alivyozungumza jibu lake mama kuwa Mabaraza haya yako 37. Nilitaka kujua tu, ndani ya Mkoa wangu wa Mjini/Magharibi Mabaraza mangapi yanayofaidika na fedha hizo zilizotolewa.

Pili, nilitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kimetumika ndani ya Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa vile suala la nyongeza la Mhe. Mwakilishi limelenga sana kwenye takwimu kwa hivyo naomba suala lake hili niweze kumjibu kwa maandishi ili tuweze kupata jibu sahihi. Ahsante.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba amesema kwa mwaka 2017/2018 wizara ilitenga jumla ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya Mabaraza ya Vijana. Pia amesema

kwamba kati ya vikundi ambavyo vimesaidiwa ni jumla ya shilingi milioni sitini na moja wamesaidiwa vikundi hivyo. Nilitaka kufahamu kwamba je, katika hizi shilingi milioni sitini na moja zimetoka katika bajeti ile ya serikali ya milioni mia moja au kwenye Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi.Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika fedha hii niliyoitaja ya shilingi 61,244,000 milioni ni fedha ambayo imetoka katika Mfuko huu wa Baraza la Vijana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza kwamba, katika fedha hizi zilitumika vipi ili kuweza kuwafikia walengwa. Na vipi ziliweza kugawiwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Vijana swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, fedha hizi zilizotolewa kwa vijana ziliweza kutumika kwanza kwa ajili ya kutafuta vifaa vya ofisi na vile vile tunavyofahamu kwamba Mabaraza yetu yote ya wilaya ni Mabaraza 11. Kwa maana hiyo, kila wilaya iliweza kuingiziwa shilingi milioni sita kwa ajili ya kupanga mipango hiyo ambayo Mabaraza imejipangia. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ningependa nimuulize swali dogo lenye kipengele (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake mama ametwambia kwamba kumetengwa shilingi milioni moja kwa ajili ya Mabaraza ya Vijana, lakini kama tunavyofahamu kwenye bajeti hii shilingi milioni moja ni kwa ajili ya Mabaraza ya Vijana ndani ya mawilaya na shehia zao. Lakini hapa pia Mabaraza hayo hayo ya Vijana huunda vikundi ambavyo ametwambia kwamba Mabaraza hayo hayahitaji kusajiliwa tena, hata vikiundwa vikundi wakati ni kitu ambacho tunafahamu kuwa si kweli. Kwa sababu vijana wakishatengeneza hivyo vikundi hutakiwa wavisajili ndipo wapatiwe hiyo mikopo na ambapo mikopo hiyo haihusiani na hii bajeti ya wilaya.

(a) Je, anawahakikishia vipi vijana hao katika fedha hii kuipata kihaki-*lillahi* katika matumizi yote mawili ya ndani ya vikundi, lakini na utendaji wa Mabaraza ndani ya wilaya na shehia zao.

(b) Ndani ya vikundi hivi ambavyo amesema havihitaji kusajiliwa tena kwenye wilaya, lakini pia tunafahamu kwamba kuna vikundi kwenye shehia. Je, kuna utaratibu gani wa usajili wa vikundi ambavyo vimo ndani ya shehia na kuweza kupata mikopo kwa ajili ya maendeleo ya vijana hao na kazi zao za kujiajiri wenyewe. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kama nilivyojibu kwenye jibu langu mama kwamba Mabaraza hayo hayahitaji tena kusajiliwa kama vikundi bali yatabaki kama ni taasisi inayoweza kufanya shughuli zake mbali mbali. Nimwambie Mhe. Mjumbe kwamba Mabaraza haya tayari yameshasajiliwa, lakini wakati yanapotaka kuomba mkopo yanaruhusiwa, isipokuwa tu huwa yanatakiwa yafuate utaratibu ule wa kujisajili na kuweza kuomba mikopo kama vikundi vyengine vinavyofanya. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 22

Mpango wa Serikali katika Kuimarisha Usafiri wa Taxi

Mhe. Suleiman Sarahani Said - Aliuliza:-

Katika Sekta ya Usafiri wa nchi kavu hasa usafiri wa *taxi* nchi nyingi duniani gari hizo huwekewa rangi maalum na namba ili kuweza kujulikana kwa urahisi na kuwahakikishia usalama abiria. Aidha, *taxi* hizo huwa na mita inayorekodi umbali wa lengo la kuwaondolea usumbufu wageni na watumiaji wa usafiri huo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuimarisha usafiri wa *taxi* ili kuwarahisishia watumiaji wa usafiri huo na usalama wao pamoja na kudhibiti mapato ya serikali kupitia kodi.

(b) Je, ni lini serikali itaanza kuboresha sekta hiyo.

(c) Je, serikali haioni kwamba inapoteza mapato katika sekta hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli katika Sekta ya Usafiri wa *Taxi*, gari huwekewa rangi maalum na namba maalum kwa ajili ya kuweza kujulikana kwa urahisi na hapa kwetu Zanzibar suala hilo linatekelezwa kama ilivyoelezwa katika Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 *(Road Transport Act).*

(a) Tayari serikali imeshaimarisha usafiri huo katika Kanuni ya 27 na 29 ya gari za biashara inazitaka gari zote zinazofanya biashara ya *Taxi* kuwa na kibati chenye rangi nyekundu na maandishi yalioandikwa kwa rangi ya njano, ili kuzitofautisha na gari nyengine katika usajili. Aidha katika milango yote ya mbele ya gari hizo zinatakiwa ziandikwe neno *Taxi* kwa herufi kubwa lenye kima kisichopungua *100mm* pamoja na idadi inayoruhusiwa kuchukua na kanuni ya 35 ya gari za biashara inazitaka gari zote zinazofanya kazi ya biashara ya *Taxi* kuwa na kibati cha maandishi juu ya bodi la gari *(Taxi roof plate),* chenye maandishi yanayosomeka kwa nyuma na mbele chenye rangi ya manjano, chenye kung'ara na kinachowaka taa wakati wa usiku ili ijulikane kwa wakati wote kwamba hiyo ni *Taxi*.

(b) Serikali tayari ishaimarisha sekta hiyo, lakini hata hivyo sasa ina mpango wa kuandaa kanuni itayoainisha gari za *Taxi* kupanga rangi ili kutofautisha wilaya zinazofanyia kazi *Taxi* hizo.

(c) Serikali haikosi mapato kwa gari zote zilizosajiliwa, kwani gari zote zinazofanya biashara ya *Taxi* kihalali zinapewa leseni ya kufanyia biashara hiyo wakati wa usajili na kitambulisho maalum *(license card).* Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini na mimi niweke swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa tunakwenda katika mfumo huu ambao utatumia alama za *Taxi* na rangi ambazo zitajulikana. Je, tutaendelea na mfumo wetu wa kupatana katika kupelekana au tutatumia kilomita kwa kulipana.

(b) Ni kwamba alisema Mhe. Naibu Waziri zitapakwa rangi na kuandikwa wilaya inayotumika. Je, *Taxi* hizo zitakuwa zinatumika katika wilaya hiyo au zitakuwa zikichukua abiria kupeleka wilaya nyengine kutakuwa na malipo fulani unalipa au ni kwa ajili ya kujulikana tu kwamba gari hii inatoka wilaya fulani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Ni kweli kama nilivyosema hapo mwanzo nchi nyingi hivi sasa zinatumia mita katika kujirekodi na baadae yule anayetumia ile *Taxi* analipa ile pesa kwa mujibu wa ile mita aliyotumia. Lakini kusema la kweli ni hatua kwa hatua. Hivi sasa tunaanza na hatua hii ya kupaka rangi gari kwa kila wilaya na baadae tutakwenda hatua hizo ili kuhakikisha kwamba mapato yanapatikana na vile vile inajulikana kiasi ambacho mwananchi anatakiwa alipe anapotoka sehemu moja kwenda nyengine.

Kuhusu kama hizi gari zitakuwa zinakwenda wilaya ile au ile, kutakuwa kuna utaratibu maalum, gari itapotoka wilaya moja kwenda wilaya nyengne kutakuwa na utaratibu ambao unatakiwa utumike kulipa angalau tunaita tozo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze madereva na wenye vyombo ambao wanasaidia wananchi wetu kwa usafiri kuanzia mashamba vijijini mpaka mjini, lakini pia niwapongeze watu wenye daladala, wenye *Taxi* kwa kusaidia sana jamii yetu ambayo inapata kwenda kwa haraka na ndio wakati tuliokuwanao.

Swali langi Mhe. Spika, tukizingatia maendeleo ya nchi ni haraka ya usafiri na kwa bahati nzuri katika Zanzibar tuna *route* nyingi katika maeneo ya mjini na vijijini. Lakini kuna vijana wetu wa bodaboda sasa hivi katika nchi yetu hii na tunaambiwa kwamba vijana wajiajiri kwa njia moja au nyengine ili kujisaidia katika maisha yao.

Je, kwa kuwa *Taxi* zimepangiwa mpango mzuri kutakuwa na Kanuni nzuri kwa usalama wa watu wetu. Waziri haoni kwamba umefika wakati sasa hivi bodaboda wakapewa vibali rasmi, hati rasmio na uthibitisho wa usalama kwa kazi zao ili kusaidia wananchi wetu na ajira kupatikana kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema hapo kabla katika Baraza lako tukufu kwa mujibu wa Sheria Nam.7 ya Mwaka 2003 kifungu 82 ina-*classify* daraja zote zile za gari ambazo zinaruhusiwa kufanya kazi hiyo ya biashara. Kwa hiyo, katika sheria yetu ile bodaboda bado hatujaiingiza, lakini kama anavyosema ni jambo ambalo linazungumzika na mpaka hivi sasa tunaendelea kukaa na wadau wahusika na pale ambapo tutaona kwamba sasa hivi imeshafika wakati baada ya kuangalia lakini vile vile faida na hasara zake.

Kwa sababu kama unavyojua bodaboda pia kuna faida na hasara zake, baadae tutaileta sheria hapa kwa ajili ya kubadilishwa baada ya kupelekwa serikalini. Ahsane Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa Naibu Waziri yeye hutumia *process* ya *West Minister* au Bunge la Uingereza basi na mimi nitamuuliza swali langu kwa lugha ya Waingereza.

(a) *Honorable Speaker in Zanzibar there have been in a greate tense the number of every body now is investing in taxi, every body wants owner taxi and the marketing becoming such rated. Every were you go all most every house hold has a taxi. Now how does the government intend to control and save the interest of this market to make sure the taxi are running their business suficiently in the right order.*

(b) In many areas when you go you will find areas that you have taxi rent, which are properly for the taxi to can park their cars, passengers can follow them. How does the government intend to make sure that areas like Tunguu and Jumbi with have enough taxi rent. Thank you very much Honorauble Speaker.

Mhe. Spika: Mheshimiwa mjibu kwa Kiswahili, tunafanya haya kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ...

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe aliyemaliza hakutumia lugha ya Baraza, kwa mujibu wa Kanuni

za Baraza kifungu 25 sio lugha ya Baraza na kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri hatakiwi kujibu swali hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakuruhusu Mheshimiwa, nakuruhusu kakae.

Waheshimiwa maswali yamekwisha nina tangazo la wageni …
NA. 4
Mhe. Spika: (anaendelea) maswali yamekwisha nina tangazo la wageni.

Wageni tulionao Waheshimiwa kwanza ni Mhe. Ussi Salum Pondeza Mbunge wa Jimbo la Chumbuni. Huyu ni mgeni wa Mhe. Miraji Khamis Mussa ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo hilo hilo. Lakini pia tunatambuwa kuwa na maswahibu wake mmoja akiwa Mhe. Issa Haji Ussi Mhe. Waziri, karibu sana Mhe. Ussi Salum Pondeza. Mgeni mwengine ni Bi. Asha Shaaban Said ambaye anatokea Bumbwisudi huyu ni mgeni wa Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini. (*Makofi*)

Waheshimiwa lakini pia pana mgeni Mhe. Khamis Yahya Machano simuoni atakuwa ameondoka Mbunge wa Jimbo la Chaani mgeni wa Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Mwakilishi wa Chaani.(*Makofi*)

Baada ya hapo Waheshimiwa nina tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa C*PA Zanzibar charter* anawatangazia Wajumbe wa *CPA* pamoja na *CWP* kikao ambacho kitafanyika chumba namba 2 baada ya hichi kipindi cha maswali na majibu.

Baada ya hapo naomba sasa nimwite sasa Mheshimiwa nimekuona.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona. Mhe. Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 42 (9) (d).

Mhe. Spika, nilikuwa na jambo ambalo linahusu *ZBC* kama umeniruhusu naomba niendelee.

Mhe. Spika: Nakuruhusu.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, jana wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu mwanasheria msomi akiwa anajumuisha au akitoa ufafanuzi juu ya suala zima la hoja ya Mhe. Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf iliyokuwa ina mkanganyiko na Mhe. Kabudi. *ZBC* hawakuonesha na walituonesha tarabu walikata. Sasa wananchi wengi walikuwa wanatumainia ile mikanganyiko hii Mhe. Mwanasheria Mkuu anaiweka sawa ili basi wawe na amani katika nchi yetu yote ya Tanzania. Lakini bahati mbaya sana *ZBC* hawakufanya hivyo.

Lakini Mhe. Spika, *ZBC* Baraza la Wawakilishi tumekuwa tuliwalipa pesa nyingi sana kwa siku kwa kuonesha vipindi vyetu. Lakini siku ya Jumatano wakati tunaanza Baraza na siku ya Alhamis hawakuonesha baadae walionesha vichale tu wakati mimi na Makamu wa Pili wa Rais tulikuwa tukihangaika tuko ndani huko.

Sasa nataka kuona je, sitaki suala hili lijadiliwe nataka suala hili serikali itoe ufafanuzi. Je, *ZBC* wameshindwa kuonesha Baraza la Wawakilishi ili pesa zile tunazozitumia kwao tuweze kukodi chombo cha nje au *ZBC* kwa makusudi imefanya jambo lile lisimuoneshe Mwanasheria Mkuu kutoa ufafanuzi vile ni *sabotage* au vipi. Naomba ufafanuzi wa serikali. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi .....

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu

Mhe. Spika: Subiri tumalize hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha nimshukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed ndugu yangu kwa maelezo yake.

Mhe. Spika, *ZBC* inajitahidi kufanya kazi zake, lakini kama chombo ambacho cha kitaaluma wakati mwengine mitambo hutokea na hitalafu na kwa msingi huo inapotokea hitilafu wao hufanya wajibu wao wa kurekebisha hitilafu hizo. Lakini wanajitahidi kufanya kazi vizuri pale inapotokea hitilafu huwa hawaifanyi kwa makusudi lakini matatizo ya mitambo.

Kwa hiyo, sie kwa upande wetu tukokee ushauri wa Mhe. Mohamed Said Mohamed ili tuzidi kukaa na wenzetu wa *ZBC* wafanye marekebisho ili waone wakati wote mitambo yao iweko hewani itusaidie kutoa matangazo yetu.

Lakini juu ya yote hayo inabidi nichukuwe fursa hii niwapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya *ZBCm* wameendelea kuwa hewani na wamefanya hivyo wakati wote na vile vile wamefanya marekebisho makubwa katika *studio* zao na kwa sasa ukiziangalia inaonekana wazi itakuwa ni moja katika *studio* za mfano katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na serikali itaendelea kuwaunga mkono ili waweze kufanyakazi zao vizuri na pale ambapo panapotokea hitilafu na kama kipindi kina umuhimu kwa namna inayotakiwa kwa wananchi iwafikie, basi serikali itachukuwa juhudi ya kuwaambia *ZBC* ili kipindi hicho kitoke na wananchi waweze kukisikia.

Nakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf: Mhe. Spika, "*Bismillah Rahman Rahiym*" na mimi nimeinuka na kanuni ya 42 lakini *concern* yangu iko katika *passport* mpya. Ningeomba kwa serikali

ije inipatie majibu kama alivyosema mwenzangu haina haja ya kujadiliwa.

Mimi toka nimepata fahamu zangu sasa hivi nina *passport* 5 za Zanzibar zote za Tanzania. *Passport* zote tulizokuwa tunazo nyuma mpaka *Diplomatic* nyeusi iliyopita hapo nyuma sehemu ya mahala pa kuzaliwa sisi Wazanzibari imendikwa Zanzibar na *PC* imekuwa *Issued Zanzibar Immigration Head Office*. Lakini hii mpya tuliyoipa nyekundu ya *Diplomatic* na watu wa kawaida imeandikwa mjini, kuna wengine wameandikiwa Kusini, kuna wengine wameandikiwa Kaskazini. Kwa nini isiandikwe Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Unguja, kitu Mjini, kitu Kusini hata ukitaka kukitaipu katika Kompuyta hakitambulikani katika *system*.

Sasa ningeomba serikali itujuulishe hivi kweli wamekaa na wenzetu Tanzania Bara kuhakikisha kwamba jina la Zanzibar halindoki kwenye *passport* kama ilivyokuwa huko nyuma?

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili au Mhe. Mwanasheria Mkuu yeyote kwenye serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi aidha nimshukuru Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa kutoa hoja yake.

Mheshimiwa inaonekana hoja yake ina maelezo ya kitaalamu kidogo kwa sababu *passport* yangu mimi imeandikwa mahala nilipozaliwa na mahala ilipotolewa Zanzibar. Kwa hiyo, ni vizuri tukapata ufafanuzi zaidi kwa watalaamu. Nilichukuwe shauri lake Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf likafanyiwe kazi tuone kosa liko wapi na marekebisho yafanyike.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti aje achukuwe kiti.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Namba 7 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na kuweka Utaratibu Bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikiliza wa Kesi za Jinai

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza michangio naomba utulivu uwepo katika Baraza ili tuendelee. Sasa namwite Mhe. Wanu Hafidh Ameir kuendelea na mjadala wetu uliko mezani.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikasema machache katika mjadala ambao ulianzia jana kuhusu Mswada wa Sheria, Sheria ya kufuta mwenendo wa Jinai namba 7, 2014 na kutunga Sheria Mpya ya mwenendo wa Jinai na kuweka utatibu bora wa kutekeleza majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini pili nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake lakini kwa namna ya pekee nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa kamati yangu ya Katiba na Sheria kwa kuupitia Mswada huu lakini pia kwa kuwasilisha hotuba kwa niaba ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla sijaingia katika vifungu vya mswada ningependa kusema mambo mawili au matatu.

Kwanza kabisa niseme kwamba naamini mswada huu wale wadau wote wahusika ambao wanahusiana na kusikiliza hizi kesi za jinai wamehusishwa. Kwa hiyo, hakutakuwa tena na yale matatizo kwamba polisi inamsingizia Mahakama na Mahakama anamsingizia *DPP* na *DPP* anasingizia mashahidi. Naamini wadau wote walikutana na wakatoa maoni. Kwa hiyo, hatutarajii kwamba kutakuwa na matatizo yale yale ambayo walikuwepo kabla.

Lakini suala jengine kwamba nipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta Miswada hii mitatu kufanyiwa marekebisho naamini kwamba sababu ni kuweka utaratibu mzuri ambao kesi zetu zitakuwa zinasikilizwa. Lakini niiombe sana Serikali ya Mapinduzi sambamba na usikilizwaji huu wa kesi ni vyema kwa kuwa wenyewe wanasheria wanasema kwamba hakuna hukumu bila ya ushahidi. Naamini kwamba na siku hizi wanachukuliwa sana ushahidi wa kisayansi kuliko wa kimazingira.

Naiomba sana Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar nazungumzia katika kesi ya ubakaji ningeomba huu urekebishaji wa hizi sheria uende sambamba na ununuliwaji wa *DNA* ili sasa ule ushahidi ambao wanasema kwamba hawaamini ushahidi wa mazingira na huwa wanataka ushahidi wa kiteknolojia uwe unafanyakazi. Kwa hiyo, niombe sana kazi wamefanya kurekebisha miswada lakini kurekebisha mswada ni moja, utendaji ni jambo jengine. Kwa hiyo, naomba sana huu urekebishwaji wa miswada uende sambamba na ununuliwaji wa *DNA* itatusaidia sana katika kesi za ubakaji.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, sitoingia sana katika mswada kwa sababu sikupata ya nafasi ya kuchangua sana huu mswada

kutokana na majukumu mengine. Lakini naamini kamati yangu imefanya kazi nzuri sana na ndio maana wakaja na hotuba ambayo wamewasilisha ambayo ilikuwa nzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa katika kifungu cha 151 kuhusu masharti na kuhusu dhamana. Naunga mkono hoja kabisa kwamba kuna baadhi ya makosa hivi sasa ni vyema yakawa hayana dhamana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi cha 151 kinatoa masharti kuhusi dhamana lakini ukiangalia 151 (4) ndio ambapo *concern* yangu ipo hakuna dhamana katika makosa yaliyoorodheshwa kwenye kifungu cha 151(1) ila 151(4) kinampa mamlaka Jaji Mkuu kutoa dhamana katika kesi yoyote.

Sasa hapa nna *concern* mbili kwanza, hatari ya kuzuia dhamana kabisa. Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua hawa washitakiwa nao binadamu na nazungumzia kuhusu makosa yale ambayo hayahusiani na uhaini na ya ubakaji. Hawa washitakiwa ni binadamu na saa nyengine mtu ana sababu tofauti za kibinadamu kwa mfano labda mtoto chini ya miaka 18 lakini pia kuna mtu anaweza akashitakiwa lakini ana maradhi ya kuambukiza. Kwa hiyo, huwezi labda kwenda kumchanganya na washitakiwa wengine. Lakini pia kuna utu uzima na "*think like that*" .

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana sheria hii iangalie iweke masharti ambayo yatakayoweza kutoa dhamana kwa baadhi ya watu wenye sababu mahasusi. Nilikuwa naomba hilo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliangalie.

Lakini *concern* yangu nyengine ni kuhusu kupewa Jaji Mkuu kupewa *Jurisdiction* yeye tu ya kutoa dhamana. Wakati Jaji Mkuu ni sawa sawa na Majaji wake wengine wanaosimamia haki, isipokuwa tu yeye ni Jaji Mkuu kuliko wale wengine ambao wapo. Sasa nilikuwa naomba na Jaji Mkuu tunajua ana kazi mbali

mbali ambazo zitakazoweza kufanya saa nyengine hayupo ama kwa namna mmoja au nyengine yeye hatoweza kufanya kazi.

Ombi langu ni kwamba wakati tunampa Jaji Mkuu *power* ya kutoa ama *Jurisdiction* ya kutoa dhamana ni vyema pia tukawapa wale majaji wengine kwa sababu hadhi yao ni sawa isipokuwa yeye tu ni Mkuu kuliko wale. Lakini pia kazi wanazotekeleza zote ni sawa sawa na wale Majaji wengine. Kwa hiyo, kuliko kumpa yeye pake yake *power* ya kutoa dhamana ni vyema tukaangalia wale majaji wengine pia wakawa na *power* ya kutoa *Jurisdiction* ya kutoa dhamana kwa kesi ambazo zinatakiwa kutolewa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwazo sikupata muda sana wa kuangalia huu mswada lakini katika kuutupia tupia macho hayo ndio mambo ambayo niliyaona katika mswada huu na namba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu aya-*consider* wakati akiwa anafanya majumuisho ya huu mswada. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa ninamwita Mhe. Asha Abdalla Mussa na yeye aweze kutoa mchango wake.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia mswada huu wa Sheria Mpya ya mwenendo wa Jinai na kuweka utaratibu ulio bora na upelekezi wa makosa ya jinai na usikilizaji wa makosa ya jinai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi lakini nianze na kuwapongeza wizara kwa kuandaa mswada huu. Lakini pia niunge mkono Kamati kwa marekebisho yao pamoja na mapendekezo ambayo wametuletea na pia niungane na Wajumbe wenzangu waliochangia mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, niseme

kwamba mswada huu tutakapoupitisha hapa itakuwa ni fimbo ya kuwachapia wale ambao wenye makosa ya jinai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazangumzia masuala ya kuhusu dhamana. Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 151 kinazungumzia masuala ya masharti kuhusu dhamana. Lakini mimi nitazaungumzia kufungu namba 151(2),(3) na (4). Mhe. Mwenyekiti, Kifungu nambari (3) kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na haitokuwa kikubwa sana. Lakini Kifungu namba (4) kinasema kwamba "Bila ya kujali chochote kilichomo katika kifungu (1) Jaji Mkuu anaweza katika kesi yoyote kuelekeza kwamba mtu yeyote apewe dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kuna makosa ambayo hayahitaji dhamana. Mhe. Mwenyekiti, makosa haya yakiwemo kuuwa, ubakaji na madawa ya kulevya pamoja na mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia masuala mazima ya ubakaji, tunafahamu sote suala la ubakaji hapa Zanzibar kila siku zinavyokwenda mbele basi masuala yanazidi. Hivi juzi tu wakati tunapitisha Sheria za Adhabu mpya baada ya kutoka hapa tu siku ya pili yake tunasikia kwamba kuna msichana wa miaka 17 amebakwa na watu wawili Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi kinazungumzia kwamba Jaji Mkuu anaweza katika kesi yoyote kusema mtu huyo apewe dhamana. Lakini mimi nina wasi wasi kwa sababu mtu utakuta amebakwa au mtoto wa miaka miwili amebakwa, lakini pia mshitakiwa huyo anakamatwa anapelekwa kituoni na anapofikishwa kituoni baada ya siku mbili mshitakiwa yule unamkuta yuko nje na hii inasababisha kumuasi mtu yule ambaye amepata na tatizo lile.

La pili, mzazi wa mtoto yule anapata athari kubwa sana. Hivi juzi tu, kuna mtoto wa miaka mitano amefanyiwa vitendo vibaya na

baba yake mzazi, baba yule akachukuliwa akapelekwa kituoni baada ya siku tatu baba mtu akawa yupo nje kwa dhamana, lakini ile kesi sasa ni muda wa miezi minne unakwenda mwezi wa tano mtoto yule ameathirika kisaikolojia lakini pia ushahidi upo unaonekana. Lakini imemsababishia mama wa mtoto yule sasa hivi amepata athari kubwa na anaweza wakati wowote anaweza kupoteza maisha yake.

Hivi vitendo vipo lakini tuviangalie kwa kina, kwa upande wangu mimi kifungu hichi mapendekezo kiondoshwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu namba 152 kinachozungumzia kwamba usikilizaji wa kesi ambayo mtu anashitakiwa kwa kosa ambalo lisilo na dhamana lazima uanze ndani ya miezi sita kutoka tarehe ya mtu ambayo ameshitakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilivyofahamu kwamba mtuhumiwa amepatikana amefanya kosa ameweka ndani lakini kesi yake haiwezi ikasikilizwa mpaka ifike miezi sita unatafutwa ushahidi, ushahidi huo ushahidi gani ambao unatafutwa ndani ya miezi sita. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti suala hili mimi kwa upande wangu napendekeza kwamba usikilizaji wa kesi baada ya mshitakiwa kupatikina basi angalau upunguzwe uwe ndani ya miezi mitatu. Kwa sababu niseme tena hivi juzi tena Mkoa huo huo wa Kaskazini Unguja, maeneo ya Mkokotoni kuna mtoto amebakwa mtoto mdogo na matokeo yake mshitakiwa akawekwa ndani akachukuliwa dhamana, na dhamana hiyo imekwenda kuchukuliwa kwa mama yake mzazi na mama mzazi huyo ni mtu mzima ambaye hafahamu lolote, lakini polisi amekwenda kumlazimisha yule mama aweze kumchukulia dhamana mtoto wake na hatimae baada ya muda mshitakiwa yule baada ya kuchukuliwa dhamana akatoroka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haya masuala yanasikitisha sana naomba sana katika kifungu hichi cha 152 basi tuone kwamba huu

muda wa kusikilizwa kesi, basi naomba upunguzwe badala ya miezi sita basi iwepo angalau miezi mitatu nadhani ushahidi wote utakuwa umepatikana na baadae mtuhumiwa anaweza kuchukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye kifungu namba 294, kifungu hichi kinazungumizia utaratibu pale mwanamke aliyetiwa hatiani kwa kosa lenye adhabu ya kifo anapodai kuwa yeye ni mja mzito. Mhe. Mwenyekiti, suala hili mimi nimefahamu kwamba pindipo mwanamke atakuwa mjamzito lakini pia amepatwa na hatia ya kuhukumiwa adhabu ya kifo, nilipokisoma nimekiona kwamba pindipo itathibitika mshitakiwa yule au mtuhumuwa huyo ni mjamzito basi kosa lake atasemehewa.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba nipongezi serikali kwa kuona kifungu hichi kwamba mwanamke naye ana haki na pia niwaombe wanaweke wenzangu ambao wanatusikiliza na ambao wapo katika jamii yetu kwa jumla, waweze kwamba kifungu hichi wasikitumie kwamba labda kifungu hichi kimesema kwamba mtu yeyote ambaye mwanamke aliyekuwa mjamzito aweze kushitakiwa au anasamehewa kwa kosa fulani, naomba kwamba wajitahidi sana wajihadhari sana wasiweze kufanya makosa haya kwa kukimbilia kwamba kipo kifungu namba 294 kinanilinda.

Mhe. Mwenyekiti kwa ujumla kabisa niseme kwamba sheria hizi tunazitunga na zinaletwa hapa Barazani tunazipitisha lakini niwaombe jamii nzima wawe makini na wajue kwamba sheria hizi zinazopitishwa hapa Barazani zinatekeleza wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti kwa haya machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.(*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha Abdalla Mussa na sasa ninamwita Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na baadae atafuatia Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mswada huu wa kufuta sheria ya mwenendo wa jinai. Kwanza nashukuru sana serikali kwa kuona kuwa ipo haja ya kuleta mswada huu na sisi tuufanyie kazi na tuupitishe uwanze kufanya kazi kwa umakini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nije moja kwa moja katika kifungu cha 37 kinachosema kuwa wakati gani mtu asichukuliwe kuwekwa kizuizini. Naomba kwa ruhusa yako nikinukuu kifungu hichi "Afisa wa polisi hatamueka kizuizini kuhusiana na kosa lolote mtu ambaye alikuwa awali chini ya kuzuizi kuhusiana na kosa hilo.

a) Isipokuwa kama anafanya hivyo kutokana na mambo ambayo yamejulikana na afisa wa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa hilo baada ya mtu huyo alipoacha kuwa chini ya kuzuizi.
b) Isipokuwa kama muda wa kutosha umepita tangu mtu huyo alipoacha kuwa chini ya kizuizi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aje anifafanulie ni muda upi wa kutosha, kwa sababu hapa naona umewekwa tu muda wa kutosha. Sasa huu muda wa kutosha sujui uko kwa vipi ili huyu mtu aliyepo kizuizini naomba ufanunuzi kwa hilo. Lakini Mhe. mwenyekiti, nije katika suala zima masharti katika dhamana kifungu cha 151 uwezo wa jumla wa kutoa dhamana .

Mhe. Mwenyekiti, najua sana serikali yangu na wizara inayohusika ina nia njema sana na ndio maana ikatuletea sheria hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunaposema kwamba makosa yasiyo na dhamana tayari katika kifungu hichi wamejumuisha ni yale makosa ambayo kwanza pale mtu yeyote asiyekuwa mtu anayetakiwa kwa kuuwa kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa

kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile na mengine mengi yaliyotajwa katika kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nijue hichi kiwango kikubwa cha madawa ya kulevywa ni kipi, na ni kiasi gani, kwa sababu hapa hatujaona kuwa kimewekwa kiwango kikubwa ni kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza kuwa tuweke kifungu hasa maalum cha kuwa hichi kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya ni kiasi gani na mapendekezo yangu yatakua kama hivi ifuatavyo:-

Kiwekwe kabisa kifungu ambacho kitaonyesha kuwa kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya kuanzia kete ishirini. Mhe. Mwenyekiti, walaji wa dawa za kulevya hawakutwi na hizo kiwango kiasi hicho hawakutwi nazo sana atakuwa na kete yake moja au mbili na humkuti nayo kwa sababu tayari anakuwa ameshaitumia. Lakini hapa tukisema kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya hatujui kiwango gani.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tayari tutaona kuwa tumeshatoa ule mwanya pia. Kwa hivyo, kama tumekusudia kutokomeza madaya ya kulevya ndani ya Zanzibar yetu au Tanzania kwa jumla basi hichi kifungu kionekane kama kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya kitakuwa ni kiasi hichi. Mhe. Mwenyekiti naomba sana hichi kifungu kiwekwe na kiainishe ni kiwango gani cha madawa ya kulevya. Kwa hivyo, kiongezwe kiwekwe kuanzia kete ishirini ndio kiwango kikubwa cha madawa ya kulevya ikiwa tunataka tuondoshe madawa lakini hapa tunazongazonga tu hatujainisha kiwango gani kikubwa cha madawa ya kulevya. Kwa hivyo Mhe. Waziri najua msikivu kwa leo atanikubalia ijapokuwa yale mengine jana juzi nilitoa mapendekezo haya mengine akanipa ufafanuzi nimeridhika, lakini kwa hili namuomba Mhe. Waziri

atakapokuja waanishe hicho kiwango na kuanzia kiwango kikubwa kiwe kete ishirini.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu hicho hicho cha 154(4). Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi cha (4) kinasema, “bila ya kujali chochote kilichomo katika kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hichi Jaji Mkuu anaweza katika kesi yoyote kueleza kwamba mtu yeyote apewe dhamana”. Mhe. Mwenyekiti, hivi kweli tumekusudia katika nchi yetu hii tuondoshe makosa haya yenye dhamana ya silaha, madawa ya kulevya, kubaka.

Mhe. Mwenyekiti hichi kifungu tayari kinaonesha kuwa kitampa mamlaka Jaji Mkuu ambaye ndiye atakayetoa dhamana wakati makosa haya hayana dhamana. Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza hichi kifungu kiondoshwe kwa sababu kama makosa ya dhamana yameanishwa huku katika vifungu vyengine, basi kama ni hivyo tumeamua kuwa tusitowe dhamana kifungu hichi kiondoshwe ili haya makosa yaonekane kabisa kuwa hayana dhamana kuliko kumpa Jaji Mkuu atoe dhamana, Jaji Mkuu naye binadamu, pengine itakuwa ni Mwanaasha Khamis Juma lakini nina mpenzi wangu hapa na yeye naweza nikamuachia Mhe. mwenyekiti.

Kwa hivyo, kama tumeamua serikali kuwa haya makosa yasiekewe dhamana, hichi kifungu cha (4) kiondoshwe. Napendekea sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu wote wasikivu hichi kifungu tukiondoshe, na kama watasema kama inawezekana mtu akasingiziwa, akafanyaje tayari katika sheria hii ikithibitika kama tayari yule aliyekamatwa hakuwa na kosa lile. Sio sheria imo humu na inaeleza kama anaweza akafungua mashitaka kwa kosa lile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hichi kifungu kiondoshwe na tena naomba sana kiondoshwe na kwa sababu hiyo tu tatakaribisha rushwa tutakaribisha kuwa watu wanajiamini anajua kuwa dhamana ipo na mtu anaweza kutoka kwa misingi hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kesi za ubakaji ni nyingi na tumelalamika sana kwa hivyo mtu anaweza akafanya hivi akajua kwa Jaji Mkuu tayari ana uwezo wa kunipa mimi dhamana. Kwa hivyo, kote hapewi lakini jaji Mkuu akiona inafaa anaweza kumpa dhamana. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti hichi kifungu kiondoke.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije katika kifungu cha 39, kifungu cha 39 tayari kinasema kuwa pale mtu anapokuwa chini ya ulinzi halali kuhusiana na kosa katika muda wa msingi unaoruhusiwa kwa ajili ya kumuhoji lakini bado hajashtakiwa kwa kosa na inaonekana kwa afisa wa polisi msimamizi wa upelelezi wa kosa hilo kwa sababu ya msingi kwamba ni muhimu mtu huyo ahojiwe zaidi (a) anaweza kuongeza muda katika kuhoji kwa kipindi kisichozidi saa nane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nipendekeze katika kifungu hichi kwa vile tayari hii kesi ipo kwa polisi au kwa afisa wa polisi. Kifungu hichi saa nane ni kidogo ijapokuwa katika kifungu cha (b) imesema kama ama kabla ya kumalizika kwa muda wa awali, muda uliongozwe kufanya maombi kwa Hakimu kwa ajili ya kuongeza zaidi.Kwa nilivyo fahamu mimi hapa tayari Hakimu ameshapewa nafasi ya kuwa kama ipo haja yeye atowe kibali cha kuidhinisha kuwa yule afisa wa polisi aongeze muda wa kuhoji.

Mhe. Mwenyekiti, naona katika sheria hii mamalaka mengi amepewa Hakimu, Hakimu katika kila sehemu mara nyingi mpaka atowe masharti yale au atowe haki Hakimu. Kwa hivyo, naomba sana wampunguzie huyu Hakimu hii kazi, kwa sababu iende kule kule katika hawa mapolisi kwa sababu saa nyengine labda waje wanipe ufafanuzi zaidi. Kwa sababu saa nyengine inawezekana huyo hakimu atakuwa ana mambo mengi na sehemu ile pale ni ya kutoa hukumu, sasa inakuwaje kuwa yeye ndie anayeandika iyo haki ya upekuzi ili polisi akafanye kazi mimi

nahisi huo mdorongo Mhe. Mwenyekiti, utakuwa mkubwa sasa tena sana. Kwa sababu tu utakuwa mkubwa sana aanze kutoka pale polisi, aanze kutafuta *process* za kumpata Hakimu mpaka aandikiwe labda sijui kuwe na taratibu gani za kurahisisha katika hizo za kutoa haki au upekuzi au katika huo muda wa kumuhoji mshitakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana naiomba serikali naomba Wizara wangaalie kwa makini kwa sababu hii fursa sana wameitoa kwa hakimu katika kila kipengele haki ya upekuzi, polisi hawezi kwenda kwenye upekuzi mpaka apate kibali kutoka kwa Hakimu. Kwa hivyo, mimi naomba sana hili suala walizingatie na wampe fursa huyu polisi waweze kufanya kazi zao kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana baada ya hayo machache niliyochangia na nadhani Mhe. Waziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu kile kifungu ambacho nilisema wakiondoe kiondolewe na nadhani wamenisikia. Mhe.Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimi tisini na nane, mbili nabakisha mpaka watakapokuja kunipa majibu sahihi ambayo ninayahoji hapo nashukuru sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Wahesimiwa Wajumbe kwanza nitowe tangazo rasmi kwamba Wajumbe wote walioko nje ya ukumbi popote walipo wafike kwa sababu tuko karibu na kuweza kupitisha vifungu kama hali itakuwa hivi hatutoweza kupitisha vifungu, nawaomba sana kama wale waliopo nje ya ukumbi wafike katika ukumbi ili tuweze kukamilisha kazi yetu iliyotuleta hapa.

Mhe. Said Soud Said ndiye atakayetumalizia kwa asubuhi hii ya leo.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu juu ya hoja hii ambayo tunaijadili hapa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hizi haziwagusi peke yao watu huko nje hata sisi tuliomo ndani ni sheria ambazo zitatulazimu kuzifuata na hatimae kuzitekeleza. Lakini pamoja na hayo kwanza nachukua nafasi ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizi kwa jitihada zake za kutaka kuona Zanzibar inakwenda kisheria na watu wote wanapata haki kwa mujibu wa sheria.

Kwa maana hiyo ni kwamba bado naandelea kusema kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Rais mtendaji na ndio maana harakati za kuifanya Zanzibar itoke pale ilipo na ipige hatua anaziendeleza siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, makosa ya jinai yataendelea kuwepo Zanzibar na sehemu nyingi za dunia, kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya dunia na jinai ni sehemu ya mazingira na mazingira yamemzunguka mwanadamu. Kwa vile makosa haya yataendelea kuwepo na ndio maana leo tumekaa kwa ajili ya kuona kwamba ipo haja sasa kuongoza vifungu vya adhabu, kuongeza utaratibu wa dhamana na hatimae ile haki iweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya dhamana ni haki ya kila mshtakiwa lakini tumesema kwamba yapo makosa sasa baadhi ya washtakiwa wasipewe dhamana. Kwa nini wasipewe dhamana, kwa sababu ya kuichafulia heshima Zanzibar pamoja na serikali yake, kuwachafulia Wazanzibari heshima na utamaduni wao waliouzowea na desturi zao. Kwa hivyo, tumesema kwamba haya makosa ya aina hii yasipewe dhamana na hiyo ni haki ya serikali pale inapoona kwamba jambo limekithiri basi kuweza kukaa na kufikiria namna ya kulizuwia kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, katika mazingira kama hayo kujenga na kuelimisha watu ni wajibu wetu sisi kama serikali, kwamba tunajenga sheria lakini pia tunapata nafasi ya kuwaelimisha watu kwamba sasa kuna hoja hii katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumzia dhamana kwa Jaji Mkuu. Kwanza nataka ieleweke kwamba serikali yoyote duniani ina mihimili mitatu. Kuna muhimili wa Bunge, Mahakama na Rais mwenyewe. Sasa Mahakama inasimamiwa na Jaji Mkuu na Jaji Mkuu ana dhamana zake katika kuiendesha taratibu za kisheria ndani ya nchi. Kwa hivyo mimi napenda kuona kwamba utaratibu tuliokuwanao Zanzibar uendelee wa kumpa heshima Jaji Mkuu awe ndiye mwenye mamlaka ya kutoa dhamana kwa yale makosa ambayo yeye ataona yanastahili kupewa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, kwa sababu utaratibu wa kubaka sheria au kuziingilia kwa mlango wa nyuma sheria unaweza kujitokeza, pindi tukitoa nafasi kwa mtu mwengine yeyote zaidi ya Jaji Mkuu. Kwa maana hiyo ni vyema tukakubali kuendelea na utaratibu wetu wa kumfanya Jaji Mkuu kwamba ndiye mwenye mamlaka pekee ya kutoa dhamana ili kuuheshimu huu muhimili wa Mahakama.

Pia ningeshauri Mhe. Mwenyekiti, kwamba watunga sheria lazima wawe na utaratibu wa kuziangalia sheria, kwa sababu watu wetu wanaopatwa na matatizo tunahitaji matatizo yale yaweze kupatiwa ufumbuzi mara moja na wajisikie kwamba wako huru ndani ya nchi yao. Sio mtu anakuwa na tatizo miaka saba au nane, kisingizio ni kwamba eti sheria au mwanasheria hajapatikana au Jaji hajakuwa na nafasi. Mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuwe tupo tayari sisi kama serikali kuyasimamia, ili kuwafanya wapiga kura hawa, maana hawa ni wapiga kura na ndio watu wanaoiweka serikali madarakani. Mtu yeyote anaweza kufanya kosa wakati wowote bila ya kutegemea kwamba atafanya kosa. Ni sawa sawa na binadamu kwamba wakati wowote naweza

kuwa mlemavu bila ya kutegemea kwamba atakuwa mlemavu. Sasa basi sheria ni lazima ziwe zina meno, zinang'ata kwa utaratibu mzuri.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni wajibu sasa wa kujiweka vizuri kwa Mwanasheria Mkuu, Jaji Mkuu na Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Zanzibar kupanga utaratibu wa kupita kwenye Magereza na kuona wananchi wale wako ndani kizuizini kwa utaratibu gani. Nasema hivyo kwa sababu, sio jambo la busara kumuweka mtu rumande miaka saba, sio jambo la busara mtu kumtoa ndani ukampeleka Mahakamani lakini akifika njiani unamrudisha unasema gari haina mafuta, hili sio jambo la busara. Sasa Jaji Mkuu, Mwendesha Mashitaka na Mwanasheria Mkuu watakuwa tayari kuliona hili na ninasema kwa ushahidi. Mimi hapa nazungumza kama Mwakilishi na ninalisema kwa ushahidi hili, watu wasiwekwe kizuizini kwa muda mrefu kwa kisingizio kisichokuwa cha msingi. Mtu akibaka tumesema asipewe dhamana, mtu akikamatwa na unga tumesema asipewe dhamana, mtu akiwa analawiti asipewe dhamana kwa nini, kwa sababu haya ni makosa ambayo katika nchi yetu hatukuyazowea. Lakini yale makosa ambayo yanamfika mwanadamu mara kwa mara, yale ni makosa ambayo hatuwezi kuyaepuka na lazima sheria zifanye maarifa yake, sheria lazima zichukuwe mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sio kuwasweka watu ndani kwa muda mrefu, wakawa wako ndani wamekaa kizuizini visingizio ni waendesha mashtaka, visingizio ni mapolisi. Lengo la kuleta *DPP* Zanzibar ni kuwapunguzia Wazanzibari adhabu ya kuwekwa ndani kinyume na utaratibu, ndio maana ya kitengo hiki cha *DPP* na ndio maana kikatafutwa mpaka kikaletwa, kwa sasa kipo katika nchi yetu kwamba watu wapate haki zao kwa wakati, watu wapate dhamana kwa wakati, watu wasiweze kupelekwa Mahakamani ovyo ovyo, jambo ambalo mimi nampongeza sana Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hili analisema kila siku

kwamba hatuko tayari kumpeleka mtu Mahakamani bila ya kuwa na ushahidi kamili. Ni kweli ndio lengo la kusudio la *DPP* kuweko Zanzibar na wakati kabla ya *DPP* hajakuwepo Zanzibar kulikuwa kuna mchezo wa kuchezea sheria, lakini baada ya kuja kwa Kitengo cha *DPP* Zanzibar tumefika pahala wananchi wameweza kupata haki zao kwa utaratibu. Sasa baadhi yao nazungumza tena wasitumie siasa katika kutenda kazi zao, wasiitumie siasa baadhi ya ma-*DPP*, nasema tena na nina ushahidi wana itikadi za kisiasa na hatuwezi kwenda katika utaratibu wa kutunga sheria, katika utaratibu wa kusimamia sheria.

Kwa hivyo, namuomba Mwanasheria Mkuu na namuomba *DPP* watu kama hawa wafukuzwe. Zanzibar haiwezi kwenda na misuguano ya kisiasa ya kila siku, Zanzibar imetulia inahitaji amani, Zanzibar watu wanataka watulie wapate haki zao, anayeshitakiwa atiwe hatiani kwa mujibu wa kosa lake na kama hana kosa aachiwe. Lakini sio kwamba *DPP* aende akakae aseme huyu kwa sababu alinikatia mikarafuu yangu basi na mimi namtia adabu, haiwezekani hiyo, kitu kama hicho hakiwezekani na ninazungumza hapa kwenye chombo cha kutunga sheria kwa maana Wazanzibari wote waelewe umuhimu wa *DPP*. *DPP* amewekwa pale kumsaidia raia asiingizwe hatiani na polisi ovyo ovyo na *DPP* wetu wa Zanzibar anasimamia hayo. Sasa hawa waliokuwa wanafanya shughuli hizi sisi tunawajua na wanafanya hivi makusudi ili kuifanya serikali ionekane mbaya, wanaipiga vita serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nasema, Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Serikali awe tayari sasa kupokea taarifa zangu za mara kwa mara, mimi kama serikali sitokubali watu kuitia lawamani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, inayojali sheria za watu na haki za watu kwa kisingizio cha kisiasa. Haya yapo na hasa kwetu Pemba. Kama Wapemba wananisikia wanisikie vizuri, kwetu Pemba haya yapo. Nasema hivi kwa maana mimi namuogopa Mwenyezi Mungu tu

basi, haimaanishi kwamba labda kuna mtu mwengine zaidi. Madhali tupo hapa tunatunga sheria na tunawatakia wananchi wa Zanzibar sheria na tunawataka Wazanzibari wapate haki zao, lazima yale maovu tuyapige vita. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ningesema tu kwamba kuna haja ya kufanya kwamba watu wanaoombewa dhamana kama haki za dhamana zitakuwa zimekubaliwa kupewa dhamana, basi ni haki yao ya msingi na ni haki yao ya kikatiba. Kwa hivyo, katika kulifanya hilo maana yake ni kwamba tunaboresha Katiba ya Zanzibar na taratibu zake za kila mtu aheshimiwe kwa utu wake. Kwa hivyo haimaanishi kwamba mtu akiwa jela au akiwa polisi utu wake umemalizika, hakuna hiyo. Mtu yeyote kwa mujibi wa Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ana haki ya kuheshimiwa utu wake.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa ninamwita Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na yeye kutoa michango yake pamoja na kusaidia kujibu baadhi ya hoja. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwa njia ya kujibu hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe waliochangia Mswada huu wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai namba saba ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kujibu hoja ya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, pamoja na mambo mengine yeye alikuwa anagusia masuala ya elimu

kutolewa katika ufikishwaji mzuri wa mswada huu baada ya kuwa sheria baada ya kusainiwa na Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, wazo ni zuri kwamba mara tu baada ya sheria hii kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni vyema elimu ikatolewa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tuelewe kwamba elimu haiko kwa upande wa serikali tu kwamba sisi serikali kwa maana ya serikali ndio ambayo inalazimika tu kutoa elimu hii kwa wananchi. Lakini tuelewe pamoja na majukumu mengine, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunao vile vile wajibu wa kutoa elimu hii katika majimbo yetu husika. Sambamba na hilo na zile taasisi mbali mbali ambazo zilizokuwa za kiserikali nao kwa njia moja au nyengine naamini kwamba elimu hii itafikishwa kwa wananchi na wananchi waelewe yale yote ambayo yaliyozungumziwa katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sambamba na Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, pia Mhe. Simai Mohamed Said Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu na yeye pia alielezea kwamba umuhimu wa elimu kutolewa ili wananchi waweze kuielewa sheria hii. Kwa hivyo, kwa sambamba niweze kusema kwamba elimu itaendelea kutolewa ili kuhakikisha wananchi wetu wanaelewa sheria mbali mbali sio hii tu.

Mhe. Mwenyekiti, mchango mwengine wa Mhe. Ali Suleiman Shihata, yeye alikigusia vile vile kifungu cha 203 ambacho kinazungumzia masuala ya adhabu ya kifo. Yeye anasema kwamba adhabu ya kifo ifutwe na amesema kwamba imepitwa na wakati. Mhe. Mwenyekiti, bado tunaendelea kusisitiza kwamba adhabu ya kifo bado tutaendelea kuwa nayo kwa sababu tunaona kwamba hii ni aina moja kama aina nyengine zilivyokuwa za adhabu. Kwa hivyo, adhabu ipo na utekelezaji wake tunauona, kwa sababu ilipotolewa adhabu ya kifo basi pale Mahakama inapoamua kutoa ile adhabu ya kifo, kwa hivyo ni njia moja ya

kwamba adhabu hii inaanza kutekelezwa. Kwa hivyo, tuelewe kwamba umuhimu wa kuwa na adhabu hii upo kuliko vile ambavyo tukasema moja kwa moja itolewe adhabu hii. Lakini kubwa zaidi nitowe wito kwa wananchi wetu tujiepushe na makosa mbali mbali, ili tusije tukaingia hatiani katika adhabu mbali mbali ikiwemo hii adhabu ya kifo, tuwe raia wema na tuendelee kuisaidia nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwa Mhe. Simai Mohamed Saidi na yeye pia alizungumzia suala la askari wapatiwe vitendea kazi katika kuweka kumbukumbu sahihi wakati wa mahojiano. Hilo nalo ni wazo zuri, wazo ambalo litapelekea ufanisi zaidi katika kazi zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha na yeye alipata fursa ya kuchangia katika kifungu cha 154 kinachohusiana na kifungu kilichompa *power* Mhe. Jaji Mkuu cha kusamehe kwa maana ya kwamba kutoa dhamana kwa yale makosa mbali mbali, yakiwemo makosa ya kubaka. Yeye Mhe. Mwanaasha alisema ni vyema adhabu hii ikaondolewa.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka haya ya Mhe. Jaji Mkuu kuondolewa ni wazo zuri, lakini bado tunaona kwamba ipo haja ya kifungu hiki kubakia, kwa sababu kama tunavyoelewa wakati mwengine inawezekana kwamba mtu suala anaweza kuzushiwa tu. Kwa hivyo, tunaweza tukasema tayari amebaka na dhamana isitolewe, lakini tumeona kwamba ipo haja kwa sababu yanaweza yakatokea mazingira mbali mbali ya mtu kusingiziwa na mambo mengine. Kwa hivyo, hii tumeiona ni njia ambayo kama mtu hakuweza kutenda kosa basi mheshimiwa huyu akapata huu uwezo wa kumtoa na kumpatia hiyo dhamana. Lakini tuelewe kwamba Mhe. Jaji Mkuu hii nafasi ambayo anapewa mtu mwenye sifa nyingi, ikiwemo hekma, busara na kujitambua. Sasa nieleze kwamba tuondowe wasi wasi na hususan kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir na yeye alisema kwamba huu uwezo ambao amepewa Mhe. Jaji

Mkuu basi vile vile waweze kupewa Majaji wengine. Kwa hivyo, niwatowe wasi wasi kwamba bado ipo haja ya huyu Mhe. Jaji Mkuu nguvu hizi akapewa yeye tu za kutoa hii dhamana na tunafanya hivi kwa kuepuka mambo mbali mbali. Kwa hivyo, tuelewe kwamba upo umuhimu wa huyu Jaji Mkuu au kifungu hiki kubakia kwamba Jaji Mkuu yeye ndiye atakuwa Jaji pekee katika kutoa dhamana hii pale ambapo itakapohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimalizie kwa kusema kwamba ni vyema wananchi tukawa tunazitii hizi sheria, kwa sababu tutakapozitii hizi sheria tutajiepusha na makosa yale ya kuingia hatiani. Kwa hivyo, kubwa zaidi wananchi sheria hizi zinapita, sheria hizi kama wajumbe wengi ambao wamechangia ni sheria ambazo zimesheheni kila aina ya sifa zina adhabu mbali mbali. Kwa hivyo, ili tuepukane na adhabu hizi ni vyema tukatii sheria na hatimaye tukawa raia wema nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache na mimi niseme kwamba naunga mkono Mswada huu wa Mwenendo wa Jinai kwa asilimia mia moja, ili uweze kufikia kama ilivyokusudiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kusema machache sana katika hoja hii ambayo ipo mbele yetu. Pia nichukuwe fursa hii ya kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamechangia. Lakini zaidi niwashukuru kamati ambao imefanyakazi kubwa sana ya kupitia mswada huu ulipokuwa mbele ya kamati kifungu kwa kifungu na ndio maana hoja ya michango hii imerahisishwa sana baada ya kamati kuja na mapendekezo ambayo ni ya msingi kabisa, na ambayo serikali imeyakubali katika hotuba ambayo Mhe. Waziri atakuja kufanya majumuisho.(*Makofi*).

Kwa hivyo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yao ambayo mingi ni michango ya kujenga, lakini

mingine ni michango ya kutaka ufafanuzi wa baadhi ya vifungu ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamevizungumza. Hoja hii Mhe. Mwenyekiti, ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe karibu saba na ile ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwenye hotuba yake.

Lakini mengi ambayo yamezungumzwa Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni ule utaratibu ambao umezungumzwa kwenye kifungu cha 151 cha mswada. Wajumbe wengi wamezungumza kwa hisia tofauti. Kuna wale ambao wamesema kifungu kibaki kama kilivyo, lakini kuna wale ambao walisema aah! tulipofika inatosha na kifungu hiki kiondoshwe na hasa kifungu cha (4) kama ule uwezo ambao amepewa Jaji Mkuu wa kutowa dhamana sasa uondoshwe na kuwe hakuna dhamana kwenye makosa haya, mimi niwaombe sana waheshimiwa Wajumbe tulitafakari vizuri sana sana suala hili natukubaliane na hoja ambayo ipo kwenye mswada ya kubaki kama watu hawa wapewe dhamana.

Kilichobaki sasa ni utaratibu na utaratibu na utaratibu huu Mhe. Mwenyekiti tumeupitia baada ya kutafakari mambo mengi ambayo yanatokea katika kuendesha na kusimamia kesi hizi, bila ya kupokonya nguvu ambazo na uwezo ambao wamepewa Mahakimu na Majaji ambao wamekuwa wakitekeleza kazi vizuri sana na kusimamia majukumu yao kwa ufanisi zaidi, lakini kwa uzito wa makosa haya Mhe. Mwenyekiti ambayo yametajwa kwenye kifungu 151. Lakini kwa kuzingatia pia kama nilivyoeleza jana wakati nikichangia hoja ya mswada wa adhabu kwamba kila mtu yuko huru mpaka pale atakapotiwa hatiani, hiyo ni misingi ya Katiba ambayo inasema kila mtu yuko huru mpaka anapotiwa hatiani, na kama mtu huyo pia yuko huru maana yake huyo mtu pia anastahiki haki ya kukupewa dhamana, sasa nani atowe dhamana ndio suala ambalo inabidi tulijadili.

Kwenye hoja ambayo yupo Mhe. Mwenyekiti, Serikali imependekeza kama dhamana ya makosa haya makubwa na mazito ya nchi yetu basi sasa yaachiwe kwa kiongozi mkuu wa

Mahakama ambaye ndiye Jaji Mkuu. Mimi nadhani hoja baada ya kutafakariwa sana hata kamati lakini hata wataalamu wameichambua na kuja hoja hii, mimi nadhani tukubaliane na hoja ambayo ipo ndani ya mswada kama tuwache kama makosa yawe hayana dhamana, kwa Jaji ambaye atasikiliza lakini yule mshitakiwa ambaye atahisi kama anataka kuomba dhamana na ni haki yake kuomba dhamana basi aombe hiyo dhamana kwa Jaji Mkuu. Mimi nadhani tukifanya hivyo tutakuwa tumetimiza mashari ya Katiba ya kuhakikisha kwamba kila mtu yupo huru mpaka pale atakapotiwa hatiani. Kwa hiyo pia atakuwa na haki na kupewa dhamana lakini dhamana yenyewe sasa aiombe kwa Mhe. Jaji Mkuu.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti alilizungumza sana Mhe. Mwenyekiti wetu Baraza Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na akaomba sana kama tuweke viwango kwenye madawa ya kulevya kiwango gani ambacho mtu anataka kukamatwa nacho. Sasa kuna mambo mawili. Kwanza kuna Sheria ili ya Usimamizi wa Madawa ya Kulevya. Lakini ya pili kuna tangazo la kisheria, tangazo Namba 65 la mwaka 2017, limetoa viwango vya madawa ya kulevya na utaratibu wake wa ushughulikiaji wa kesi hizo. Sasa nimuombe sana Mhe. Mwanaaasha kama tayari kuna viwango ambavyo vimewekwa kupitia tangazo hili la Sheria Namba 65 la mwaka 2017.

Lakini mbali ya hiyo hata kwenye mswada ambao unapendekezwa kifungu cha 388 kimetoa uwezo kwa Jaji Mkuu nae pia kutunga Kanuni za jumla katika usimamizi wa sheria hii. Kwa hivyo kama akiisoma Mhe. Mwanaasha na akiiona, kiwango ambacho kimewekwa kwenye tangaza la Namba 65 la mwaka 2017 halitoshi basi anaweza kujenga hoja na kumshauri Jaji Mkuu pale atapotunga Kanuni za jumla za kusimamia sheria hii basi na hivyo viwango pia *revise* ambavyo sasa vitakuwa sasa vipo kwenye sheria hii! tangazo lakini pia viko kwenye sheria hii .

Kwa hivyo kiujumla Mhe. Mwenyekiti tuwashukuru sana wale ambao wamechangia lakini niwaombe sana waheshimiwa Wajumbe kwamba tukubaliane na hoja hii ambayo ipo mbele yetu na tuupitishe mswada huu wa kusimamia masuala ya mwendo wa jinai kwa asili mia moja na tuwape sasa kazi Mapolisi wetu ambao ndio wapelelezi lakini Mahakimu na Majaji wetu ambao wanatakiwa kutowa haki kwa mujibu wa Sheria, ili sasa wakasimamie haki hii vizuri na kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia moja.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kunijaalia kusimama hapa kwenye Baraza letu hili mbele ya wajumbe, natumia nafasi hii ya kutoa majumuisho kwa mswada unaohusiana na masuala ya kesi za jinai.

Mhe. Mwenyekiti jumla ya wajumbe waliochangia ni 12, Wajumbe 11 wamechangi njia kwa kusema na mmoja kwa maandishi. Idadi hii ndogo inatokama na mswada weu uliopita umechagiwa na watu wengi sana, na umechangiwa kwa sababu ulifanyiwa kazi kubwa sana na wajumbe wote. Kwa hivyo mswada umekuwa rahisi kwa sababu taarifa nyingi na taaluma nyingi zilitolewa katika mswda ule uliopita. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwataja wajumbe wote ambao wamechangi mswada huu:-

1. Mhe. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Simai Mohamed Said

4. Mhe. Suleiman Sarahani Said
5. Mhe. Shehe Hamad Mattar
6. Mhe. Wanu Khafidh Ameir
7. Mhe. Asha Abdalla Mussa
8. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
9. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
10. Mhe. Khamis Juma Maalim - Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma
11. Mhe. Mwanasheri Mkuu

12. Mhe. Harous Said Suliman – amechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekitim, nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wote waliochangia, wamechangia wametusaidia sana kufanya mswada wetu huu kuwa bora zaidi. Lakini la pili nichukuwe nafasi hii adhimu kushukuru Kamati yetu hii ya Baaza la Wawakilishi ya Katiba Sheri na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Machano Othman Said kwa kweli kamati imefanya kazi sana sana.

Jana nilipokuwa nafanya majumuisho nilisema hapa kwamba kamati ilitoa mapendekezi mengi sana kwenye mswada ule wa adhabu, nikasema kwa mara ya mwanzo si aghalabu kwamba mambo yote yanayorekebishwa na kamati au Mwenyekiti akawasilisha hapa tukayakubali yote asilimia moja, lakini jana tuliyakubali kwa asili mia moja na leo hii nasema tena marekebisho yao na mapendekezo yao yote tumeyachukuwa na tumeyakubali.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti nichukuwe nafasi hii kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri anazozoendelea kufanya na anazotusaidia katika Serikali yetu, lakini kama kawaida Mwanasheria Mkuu hafanyikazi peke yake ana wasaidizi wake wote wa ofisi. Nichukuwe nafasi hii maalum kumshukuru

Mkurugenzi wa Mashtaka ndugu Ibrahim Mzee amekuwa chachu na mwalimu mzuri sana wa kutoa taaluma juu ya masualal mbali mbali ya sheria, yeye pamoja na wasidizi wake wote. Kama kawaida naendelea kumshukuru sana Naibu Waziri Mhe. Khamis Juma Maalim kwa kazi nzuri anazoendelea kutuisaidia na kunisaidia mimi.

Mwisho niwashukuru sana wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochangia mswada huu, kutokana na hayo na kutokana maelezo mazuri sana yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri na yale ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameyasema. Kwa hivyo sitokuwa na haja ya kuchukuwa muda mrefu sana isipokuwa nataka niseme mambo mawili tu Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kwanza suala la dhamana limezungumziwa kwa uzuri sana na Mwanasheria Mkuu. Nasema Jaji Mkuu ni mkuu wa muhimili wa Mahakama na lazima tumuamini. Kwa hivyo sioni sababu yoyote kwamba tumpunguzie nguvu zake, tumpunguzie dhamana zake, nahisi tuendelee kumuamini.

Lakini la pili, nashukuru sana Mhe. Suleiman Ali Suleiman amesema na wengine na hili naliunga mkono, taaluma ni kitu muhimu sana tuendee kuitoa kwa jamii, waelewe miswada hii waelewe sheria zetu hizi nasi kwa sheria hizi ni kwa sheria zetu zote ni vizuri sana tukaendelea kutoa taaluma na tutajitahidi kwa upande wetu sisi, kwa sababu miswada hii imekuja baada ya kilio cha siku nyingi kwa wananchi wetu na tumehisi kwamba sasa hivi vilio vyao vimenyamazishwa.

Baada ya hayo machache mimi niwashukuru wajumbe wote. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mhe. Waziri ametoa hoja na hoja imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri. Wanaopinga, Wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, kanuni yetu…

Mhe. Mwenyekiti: Sijakuruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haijatimia *quorum* hii wahesabu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswaada wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai ya Mwaka 2018

SEHEMU YA KWANZA

Utangulizi

Kifungu cha 1 - 3 Pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti asogeze *microphone* karibu.

SEHEMU YA PILI

Uwezo wa Mahakama

Kifungu cha 4 – 11 Pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA TATU

Masharti ya jumla kuhusu kukamata, kutoroka na kukamata tena

Kifungu cha 12 – 54 Pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA NNE

Kuzuia Makosa

Kifungu cha 55 – 78 Pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA TANO

Masharti yanayohusiana na upelelezi wote wa jinai

Kifungu cha 79 – 103

SEHEMU YA SITA

Ufunguaji wa kesi

Kifungu cha 104 - 106

SEHEMU YA SABA

Hati za Kuwalazimisha Washtakiwa kufrika Mahkamani

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitoa hoja kwamba kwa nini sheria inampa Jaji Mkuu haki ya kutoa dhamana peke yake wakati kazi ambazo Jaji Mkuu anafanya ndio kazi ambazo Majaji wengine wanafanya. Ni kwanini sheria inampa haki Jaji Mkuu peke yake kutoa dhamana na je, Jaji Mkuu akiwa hayupo na kuna mtu anatakiwa apewe haki yake ya dhamana, nani atafanya kazi hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kutoka kwa Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kumshukuru Mhe. Mjumbe kweli wakati akichangia alisema hivyo lakini tulipofanya majumuisho alikuwa hayupo. Lakini Mwanasheria Mkuu alitoa maelezo kwa kina kabisa *(Makofi).*

Kwa hivyo maelezo hayo yameshatolewa hakuna haja ya kuyarejea tena. (*Makofi*).

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kweli wakati unafanya majumuisho nilikuwa sipo lakini kutokana kazi ambayo Mhe. Spika alitangaza pale Kamati ya Sheria ndogo ndogo ikutane juu ndio ndio maana nikawa sipo katika Ukumbi. Na nilihoji kwa nini mnatupa kazi wakati kikao kikubwa kinaendelea, bado naomba majibu kutoka kwa Serikali.

Kwa nini Sheria inampa dhamana Jaji Mkuu peke yake wakati Jaji Mkuu na Majaji wale wengine wote haki sawa sawa na kazi zao wanazofanya ni sawa sawa, yeye anasimama tu kama Jaji Mkuu ili kuwasimamia wale Majaji wengine na Mahakimu wa chini, kwa dhamana isifutwe kwa Mahakimu tu na wengine wanaoshuka chini na ibaki vile vile dhamana ibaki kwa Majaji na Jaji Mkuu. Je, Jaji Mkuu akiwa hayupo suali langu na kuna mtu anatakiwa apate haki yake ya dhamana ana kila masharti anayokidhi kupata

haki. Je, hawaoni kwamba watamnyima haki mtu yule ambaye anatakiwa apate haki yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba nichukuwe nafasi kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala la Mhe. Wanu Hafidh Amer analiuliza juu ya haki na mamlaka ambayo amepewa Jaji Mkuu katika kutoa dhamana na hoja ya Mhe. Jaku *(Makofi).*

Hoja ya Mhe. Wanu Hafidh Ameir ni kwamba kwa nini apewe Jaji Mkuu wasipewe Majaji wa Mahakama Kuu na hoja yake kubwa ni kwamba Jaji Mkuu anaweza akawa hayupo.

Kimsingi ni kwanza Jaji ndiye *head* wa ile Taasisi ya ule muhimili wenyewe. Muhimili wa Mahakama Mkuu wao ni Jaji Mkuu lakini Jaji Mkuu anapewa mamlaka haya kisheria. Jaji Mkuu ana mamlaka ya kutunga *regulation* za uendeshaji wa Mahakama, Jaji Mkuu anamlaka ya kutoa *circular* katika uendeshaji wa mfumo wa Mahakama lakini pia Jaji Mkuu anapokuwa hayupo utaratibu wetu kwamba, kunakuwa kuna Jaji wa Mahkama Kuu ambaye anaapishwa Kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu. *(Makofi).*

Kwa hivyo Jaji Mkuu muda wote itakapokuwa Taasisi au chombo cha Mahakama kinafanyakazi kila wakati na Jaji Mkuu ataendelea kuwepo. Na madhumuni ya kupeleka dhamana hii kumbakishia yeye Jaji Mkuu ni kwa sababu mbili.

1. Yametazamwa uzo wa makosa yenyewe, ukitazama uzito wa makosa yenyewe unapaswa kuwa na tahadhari kwamba nani wakumpa dhamana ya kutoa kwa ajili ya kutoa fursa yule mtu ambaye anatuhumiwa.

2. Yeye kama kiongozi atakuwa anabeba ile dhima ya kuweza kuongoza kwa kiasi gani atakuwa lile jambo mazingira yana ulazimisha kutoa ile dhamana. Kwa sababu kimsingi makosa haya kwa lugha nyengine ni kwamba hayana dhamana. Inapotokea kwamba kuna mazingatio maalum yeye Jaji Mkuu kwa kutambua dhima ya ukubwa alionao kama mkuu wa muhimili na mamlaka ambayo aliyopewa kisheria, yeye mwenyewe ndio anabeba dhima ya kutoa dhama hiyo, kwa kutambua makosa yenyewe hayakuwa yakistahiki kupewa dhamana, lakini yeye kwa kutizama mazingira yenyewe yalivyo ndio sababu ikwekwa kifungu hivyo. Vyenginevyo tukisema kwamba kila Jaji awe na nafasi hii, maana yake haya makosa tumekuwa tumeyaruhusu kwamba makosa haya nayo ni makosa ya kupewa dhamana kama yalivyo makosa mengine. Msingi kwamba makosa haya sio makosa ya dhamana isipokuwa kwa mazingira maalum, Jaji Mkuu atakuwa amepewa hiyo fursa ya kuweza kutoa dhamana ili kumsaidia Mtuhumiwa huyo kuweza kupata hiyo fursa hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria chini ya kifungu hichi. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku eeh! ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwanza naomba niweke *hansard* sawa naitwa Wanu Hafidh Ameir sio Jaku.

Na kweli nimeamini Jaku anawaumiza vichwa.*(Makofi/Kicheko*).

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake na mimi nataka niseme tu kwa hoja ile ile ambayo amesema kwamba Jaji Mkuu anapokuwa hayupo huchaguliwa mtu mmoja katika wale Majaji ambaye anaapishwa na anakuwa Jaji Mkuu, hii

ina maana kwamba Jaji yeyote anaweza kuwa Jaji Mkuu na ndiyo maana nikawa nasema kwa nini wampe hadhi yeye tu Jaji Mkuu wakati Jaji yeyote *can be a Chief Justice*.

Mhe. Mwanyekiti, sitaki kubishana sana nakubali hoja ya Mhe. Waziri lakini pia maelezo mengine nilipata chemba. Kwa hivyo nakubaliana na hayo maelezo yao lakini waangalie utaratibu mzuri ambao wataweka ili tuone kwamba hata mshitakiwa na yeye ana haki zake ambazo anatakiwa kupata, hata kama ni mshitakiwa lakini ana haki ambazo anatakiwa kupata kama mtu mwengine yeyote.

Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

SEHEMU YA SITA

Ufunguaji wa Kesi

SEHEMU YA SABA

Hati za Kuwalazimisha Washtakiwa Kufika Mahakamani

Kifungu 107 -199 Pamoja na Marekebisho Yake

SEHEMU YA NANE

Utaratibu wa Kuchukua na Kurekodi Ushahidi Katika Uchunguzi na Usikilizaji wa Kesi

Kifungu 200 - 205 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA TISA

Utaratibu Katika Usikilizaji Kesi Mbele ya Mahakama za Chini

Kifungu 206 -224 Pamoja na Marekebisho Yake

SEHEMU YA KUMI

Utaratibu Katika Usikilizaji Kesi Mbele Ya Mahakama Kuu

Kifungu 225 -274 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Kifungu 275 -291 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Adhabu na Utekelezaji Wake

Kifungu 292 - 335 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Kurejesha Mali

Kifungu 336 - 337 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA KUMI NA NNE

Rufaa Kwa Ujumla

Kifungu 338 - 369 Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA KUMI NA TANO

Upelelezi Wa Vifo Vya Ghafla Na Uchunguzi Wa Vifo

Kifungu 370 - 374

SEHEMU YA KUMI NA SITA

Maelekezo Ya Habeas Corpus Na Amri Nyengine Za Kipekee

Kifungu 375 -377 Pamoja na Marekebisho Yake

SEHEMU YA KUMI NA SABA

Mwenendo Wa Kesi Usiofuata Utaratibu

Kifungu 378 - 381

SEHEMU YA KUMI NA NANE

Mengineyo

Kifungu 382 - 390 Pamoja Na Marekebisho Yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Otawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu, na kukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba niwahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(*Hoja ilitolewa iamuliwa*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

Mswada Wa Sheria Ya Adhabu Ya 2018

(*Kusomwa kwa mara ya Tatu*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Otawala Bora:
Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai namba 7 ya mwaka 2004, na kutunga sheria mpya ya mwenendo wa jinai na kuweka utaratibu bora wa upelelezi wa makosa ya jinai na usikilizaji wa kesi za jinai na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba usome kwa mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(*Hoja ilitolewa iliamuliwa*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Kwanza sina budi nitoe shukurani Waheshimiwa Wajumbe, kuweza kujadili na hatimae kuupitisha mswada huu pamoja na marekebisho yake na kubakia hatua zilizobakia. Sasa naomba liakhirishwe Baraza hili kwa kuwa shughuli zetu za leo zimemaliza hadi kesho saa tatu panapo majaaliwa.

(Saa 5:27 mchana Baraza liliahirishwa
mpaka tarehe 14/02/2018 saa 3:00 asubuhi)